

# **Siku 40 za Maombi**

**Mradi wa  
Ari ya Uamsho na Matengenezo  
*wa Kanisa la Waadventista wa Sabato.***

Mei 3 hadi Juni 11 2022

***Uamsho***

& MATENGENEZON

Masomo haya yameandaliwa na Chama cha Wachungaji  
Konferensi Kuu ya Kanisa la Waadventista wa Sabato  
Mradi wa Ari ya Uamsho na Matengenezo  
kwa Kushirikiana na Kamati ya Uamsho na Matengenezo  
kwa ajili ya matumizi ya kanisa pamoja na mtu mmoja mmoja.  
Yameandikwa na waandishi mbali mbali kwa ari ya  
Kuombea Ulimwengu.

Tembelea <https://revivalandreformation.org/40days> kwa taarifa zaidi.

Mafungu yote yamenukuliwa  
kutoka katika toleo la Swahili Union version Bible.

Mtafsiri: Moseti Chacha (+255 712 282 224)  
Wahariri: Pr. Hebert Nziku – Katibu wa Chama cha Wachungaji STUM  
Na Pr. Daniel Ndieggi – Katibu nwa Chama cha Wachungaji NTUC

# **Yaliyomo**

<b>Juma la 1:</b> Uamsho na Matengenezo .....	4
Kabla ya Kuanza .....	6
Siku ya kwanza .....	9
Siku ya Pili .....	10
Siku ya Tatu .....	11
Siku ya Nne .....	12
Siku ya Tano .....	15
Siku ya Sita .....	15
<b>Juma la 2:</b> Siku ya Saba .....	16
Siku ya Nane .....	19
Siku ya Tisa .....	20
Siku ya Kumi .....	21
Siku ya Kumi na Moja .....	23
Siku ya Kumi na Mbili .....	25
Siku ya Kumi na Tatu .....	26
<b>Juma la 3:</b> Siku ya Kumi na Nne .....	27
Siku ya Kumi na Tano .....	29
Siku ya Kumi na Sita .....	31
Siku ya Kumi na Saba .....	32
Siku ya Kumi na Nane .....	33
Siku ya Kumi na Tisa .....	36
Siku ya Ishirini .....	36
<b>Juma la 4:</b> Siku ya Ishirini na Moja .....	37
Siku ya Ishirini na Mbili .....	40
Siku ya Ishirini na Tatu .....	41
Siku ya Ishirini na Nne .....	42
Siku ya Ishirini na Tano .....	44
Siku ya Ishirini na Sita .....	46
Siku ya Ishirini na Saba .....	47
<b>Juma la 5:</b> Siku ya Ishirini na Nane .....	47
Siku ya Ishirini na Tisa .....	50
Siku ya Thelathini .....	51
Siku ya Thelathini na Moja .....	53
Siku ya Thelathini na Mbili .....	54

Siku ya Thelathini na Tatu .....	57
Siku ya Thelathini na Nne .....	57
<b>Juma la 6:</b> Siku ya Thelathini na Tano .....	58
Siku ya Thelathini na Sita .....	60
Siku ya Thelathini na Saba .....	62
Siku ya Thelathini na Nane .....	53
Siku ya Thelathini na Tisa .....	64
Siku ya Arobaini .....	67

**Juma la 1: Mei 3 – 8**

## **Mada: Uamsho na Matengenezo**

**Karibu katika siku 40 za maombi!**

Ni wakati wa kuwa tayari kwa ajili ya safari ya kushangaza!

Kadiri tunavyojiandaa kuanza siku arobaini za maombi pamoja (yaani kuanzia tarehe 3 May hadi June 11, 2022), omba kwamba Mungu autayarische moyo wako na kwamba akuvushe ng'ambo kutoka mahali ulipo hadi katika hali yenye uzoefu ulio hai na wenye mtetemo pamoja na Yesu.

**Tunatazamia nini?**

- Kila **Jumatatu** utapokea kesha lenye kutia moyo. Kesha la kwanza likiwa limeandikwa na mchungaji Don McLafferty na kushirikishwa hapa chini.
- Siku ya **Jumanne hadi Alhamisi** utapokea kipengele cha “Changamoto ya moyo” kila siku na kupendekeza mambo ya kuombea siku hiyo. Haya mambo ya kuombea ni ya kukusaidia kuanza kuomba. Omba kwa namna ambayo Roho Mtakatifu atakuongoza.
- Siku ya Ijumaa utapokea ushuhuda wa maombi wa kutia moyo, pamoja na mambo ya kuombea kwa ajili ya mwisho wa juma.

Ni rahisi kiasi hicho. Unaweza kuanza safari hii wewe mwenyewe, ukiwa na kanisa lako, au ukiwa na Rafiki yako. Ni vyema kuwa na wenzi wa kuomba nao, kwa hiyo omba kuhusu yule utakayemkaribisha muandamane katika safari hiyo.

Njia nne za kuweza kushiriki kwa kina uzoefu wa maombi haya ya siku 40.

1. **Chimba ndani zaidi:** omba, jifunze, sikiliza kuhusu uamsho na matengenezo utakaopewa kila juma. Haya yamechaguliwa kimkakati ili kukusaidia kuzama zaidi katika mada ya juma husika.
2. **Chagua majina 7:** omba na kumwambia Mungu akuoneshe ni nani utakayemwombea katika siku hizi 40 za maombi. Andaa orodha na kuiweka katika simu yako, au uiandike mahali fulani, na kuhakikisha majina hayo yako

mahali ambapo unaweza kuyafikia na kuyaona kwa urahisi. Pengine weka namna ya kujikumbusha kwenye simu yako, au kwenye kalenda yako ili uwaombee kwa majina hawa watu 7 kila siku husika. Dai ahadi iliyoko katika Yohana 5:14 – 16 kadiri unavyoomba kila siku na usubiri na kutazamia kile ambacho Mungu atatenda kama jibu kwa maombi hayo ya dhati.

3. **Ombo na wengine:** jiunganishe na chumba cha maombi ya saa 24 kwenye mtandao kwa angalau dakika 30 kila siku ukishiriki na waumini wengine katika siku hizi 40 za maombi kwenye tovutii hii: <https://247unitedprayer.org>
4. **Funga milo mikubwa:** Ombo kuhusu uwezekano wa kuweka pembedi baadhi ya mambo katika siku hizo 40 ili kwamba uweze kusikiliza wito wa Mungu kwa uwazi zaidi na kuitikia sauti yake. Hatukushauri kuepuka kula chakula, bali pengine unaweza kuguswa kuzima televisheni yako, kujiepusha na mitandao ya kijamii, kujaribu kadiri iwezekanavyo kuachana na maburudhisho yote, vyakula vitamu vitamu, au baadhi ya shughuli ambazo unahisi kwamba mvuto wa Mungu unakuepusha katika siku hizo za maombi. Lakini kama mtu fulani alivyosema kwamba, “Tunafunga kutoka kwenye ulimwengu ili tuweze kusherehekea pamoja na Kristo.”

Je ni haja yako ya dhati ya moyo kusherehekea pamoja na Kristo? Ikiwa ni hivyo basi, Mungu ana mambo maalum aliyokutunzia katika siku hizi 40 za maombi.

Leo basi, mwombe Mungu akuoneshe kile anachotaka kutoka kwako katika siku hizi 40 za maombi kadiri unavyosoma changamoto ifuatayo ya kutia moyo, “Mungu Bado Anaita.”

Maombi kwa ajili ya safari yako,

Timu ya Uamsho na Matengenezo.

## Kabla ya Kuanza – May 2 – Wazo la Kesha

### **“Mungu Bado Anaita”**

Na Don McLattery

Siku zote Mungu anaita watu wake waje kwake. Biblia imejawa na visa vya wale ambao wameitikia wito na wale waliokataa wito.

Mungu aliwaita Adam na Hawa, nao wakajifisha (Mwanzo 3:9, 10)

Mungu alimwita Nuhu ajenge safina ili kujiokoa kutoka kwenye gharika, dunia ya wakati huo ilisema gharika haitakuja. (Mwanzo 6:14-22)

Mungu alimwita Ibrahimu na Sara nao wakaacha familia zao, wakatoka nyumbani kwao na hata kwenye nchi yao. (Mwanzo 12:1-4)

Mungu alimwita Yakobo, naye akamenyana na kulia kwamba, “Sikuachi, usiponibariki.” (Mwanzo 32:26)

Mungu aliita, na Musa akaanza kwa kutoa visingizio, kisha akamwambia Farao kwamba “Waacie watu wangu waende...” (Kutoka 8:20-32)

Mungu aliita, na Yoshua akapomoka kiusouso hata nchi, naye akasujudu, kisha akauzunguka mji wa Yeriko mara kumi na tatu. (Yoshua 5:14 – 6:15)

Mungu aliita, na Gideon akaharibu madhabahu za Baali, akapiga tarumbeta, na kuwafukuzia mbali Wamidia (Waamuzi 6:27 – 7:22)

Mungu alita, na Samweli akakimbia kwenda kwa Eli mara tatu kabla hajajibu kuwa, “Sema Bwana, Mtumishi wako anasikia.” (1 Samweli 3:10)

Mungu aliita, na Eliya akakabiliana na Israeli kwenye mlima Karmeli, akajenga upya madhabau ya Mungu na kuomba ili moto ushuke. (1 Wafalme 18:21-38)

Mungu aliita, na Yona akakimbia, katika kukimbia kwake, akamezwa na Samaki, kisha akauelekeza Ninawi katika hukumu. (Yona 1-4)

Mungu aliita, na Isaya akanong'ona kwa kicho akisema kuwa, "Nipo Bwana, nitume mimi!" (Isaya 6:8)

Mungu aliita, na Filipo akaenda mbio kwenye gari lile la Mkushi na kumfanya mwanafunzi wa Yesu (Matendo 8:29, 30)

Mungu aliita, na Sauli wa Taso akamuuliza kuwa, "U nani wewe, Bwana?" akafunga siku tatu, kisha akamtamka yule aliyekuwa akimchukia kuwa "Mwana wa Mungu." (Matendo 9:5-9, 20)

Mungu aliita, na Anania akaenda akamwekea mikono mtu ambaye alikuwa amekuja ili kumtesa, naye akasema kuwa, "Ndugu Sauli, Bwana amenitura, Yesu, yeze aliyejutokea katika njia uliyoijia, upate kuona tena, ukajazwe Roho Mtakatifu." (Matendo 9:10-17)

Mungu aliita, na Petro akahatarisha huduma yake na hadhi yake ya kumhubiri Yesu kwa Kornelio aliyekuwa na kiu. (Matendo 10:9-48)

Mungu aliita, na Yohana akaanguka miguuni pa Yesu "kama mtu aliyejufa" (Ufunuo 1:17)

Katika barua ya upendo ya Yesu, anawaita watu wake wa siku za mwisho akiwa nje – akitafuta kufika pale panapomstahili kuwa, ndani ya mioyo yetu akisema kuwa, "Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeze pamoja nami." (Ufunuo 3:20)

Huu ndio wito wake sasa kwa watu wote – Watoto, vijana, watu wazima. Ikiwa tunasubiri wito mwingine, hivi karibuni tutagundua kwamba tumeshachelewa. Anakuita wewe na mimi kwa upendo wote wa Mungu na Baba yetu. Upendo wake kama Mwokozi na Bwana, na upendo wa Roho Mtakatifu.

Huu ni wito wake ili tupate uamsho binafsi na ushuhuda binafsi. Katika vizazi vyote amekuwa akiwaita watu wake. Sasa hivi ukali wa sauti yake umeongezeka, kwani anasema kuwa, "Naja upesi..." (Ufunuo 22:7). Amekuwa akiandaa mahali huko mbingni ili tuwe pamoja naye pale alipo. (Yohana 14:3)

Wakati unaisha. Huu siyo wakati wa kuitikia wito wake kwa kujificha kama Adam na Hawa walivyofanya. Huu siyo wakati wa kujichanganya kwa sauti kama tunavyosoma kuhusu Samweli kuwa, "Samweli alikuwa hamjui Bwana bado, na neno la Bwana

liliwa bado halijafunuliwa kwake." (1 Samweli 3:7). Huu siyo wakati wa kukimbilia maeneo ambayo hatukutumwa kama Yona alivyokimbia.

Sasa ni wakati wa kunanguka miguuni pake kama mtu aliyekufa kama alivyofanya Yohana mbele za Yesu Kristo, na kurudi kwake, turudi kwenye madhabahu na kumwabudu yeye aliye Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

Mungu bado anaita, na leo hii anakuita.

*Don MacLafferty ni mwanzilishi na mwenyekiti wa Ulanafunzi. Mungu amegusa mioyo ya Don na mke wake April kuwaita vijana na wazee washiriki katika uamsho wa kila siku na Yesu kupitia katika nguvu za Roho Mtakatifu. Wanahamasisha makanisa na mashule kuungana katika kuwezesha wazazi wawafanye Watoto wao kuwa wanafunzi na kuwaandaa kwa ajili ya utume.*

### **Changamoto ya Moyo.**

Kuna sababu yako wewe kusoma maneno hayo juu hapo. Mungu anaongoza matukio katika Maisha yako ili kuwepo na fursa ya pekee ya kusikia wito wake. Wito wake umekuja kwako leo. Ni wito wa kuingia katika uzoefu wa kina ulio hai wa uamsho binafsi pamoja naye. Ni wito wa kumfuata Yesu popote anapoongoza. Je, uko tayari kuitikia wito huo?

Uko tayari kufuata wito wake leo, wito wa kina na mtetemo ulio hai, wa kwake yeye na Neno lake.?

### **Mambo 10 ya Kuombea – Kadiri unavyoandaa moyo wako kwa maombi ya siku 40**

- Omnia kwamba Mungu aandae moyo wako kwa kile anachotaka kufanya kwako.
- Omnia kwamba upate utambue wito binafsi wa Mungu wenye upendo katika Maisha yako.
- Omnia kwamba Neno la Mungu liwe hai na halisi katika Maisha yako.
- Omnia kwamba uweze kusikia sauti ya Mungu ikizungumza na moyo wako binafsi kila siku.
- Omnia kwamba maombi hayo yawe pumzi halisi ya nafsi yako
- Omnia juu ya Zaburi 139:23-24
- Omnia kwamba Mungu akupatie ujasiri na nguvu ya kuondoa mambo yote yanayokuwa vikwazo katika Maisha yako, yale yanaoyokuzuia usisikie sauti yake siku hizi 40 za maombi.

- Omba kwamba Roho Mtakatifu akupatie kutembea na Yesu kwa kina na kwa namna iliyo hai yenye mtetemo. Omba kuhusu wale utakaowakaribisha kuijunga nawe kwenye maombi katika siku hizi 40 za maombi
- Omba kuhusu majina yale 7 ya kuombea katika siku hizi 40 za maombi.

**Vyanzo vingine vya kukusaidia kuingia kwa kina.**

[Clearing the Way for the Holy Spirit – PDF Resource](#)

**Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

### Siku ya Kwanza – May 3

**Uamsho wa Uungu wa Kwali.**

“Je! Hutaki kurudi na kutuhuisha, Watu wako wakufurahie?” – Zaburi 85:6

*Uamsho wa uungu wa kweli kati yetu ndilo hitaji letu kuu na la haraka. Hii ndiyo inatakiwa kuwa kazi yetu ya kwanza. Ni lazima kuwe na jitihada za dhati za kupata mibaraka ya Bwana, siyo kwa sababu Mungu hayuko tayari kutupatia mibara yake, bali kwa sababu sisi wenyewew hatuko tayari kuipokea. Baba yetu wa mbinguni yuko tayari kuwapatia Roho wake Mtakatifu wale wanaomwomba, kuliko wazazi wa kidunia walivyo tayari kuwapatia watoto wao vipawa vilivyo vyema. lakini ni kazi yetu inayotakiwa kufanyika kwa toba, kujidhili, kuungama, na kwa maombi ya dhati ili kutimiza masharti ambayo yanahitajika ili Mungu atupatie mibaraka yake aliyolahidi. Ni lazima kutazamia uamsho kama majibu kwa maombi hayo. SM, uk. 121*

**Changamoto ya Moyo.**

Mungu ndiye chanzo pekee cha uamsho wa kweli. Uamsho ndilo hitaji letu kuu na la haraka. Je, unahisi ndani yako hitaji hilo la uamsho wa kweli? Umeshatambua uharaka wake? Unaamini kwamba Baba yuko tayari kukupatia Roho wake Mtakatifu? Bila kujali mahali ulipo au hali ya kufa unayohisi, jipe moyo na kuamini ahadi zake. Ukweli wenye nguvu ni kwamba Mungu wetu ana uwezo wa kufufua. Anaweza kutufufua tena, kurejesha uhai wetu wa kiroho tena.

Je, utamlilia leo kwa ajili ya uamsho binafsi?

**Mambo ya Kuombea**

- Omba kwa ajili ya uamsho binafsi na usiachie hadi Mungu atakapojobu

- Omba kwamba ikiwa kuna kitu kinachomzuia Mungu asifanye kazi ya kina katika maisha yako, basi akidhihirishe kwako.
- Ombea ile orodha ya majina 7 kila mmoja kwa jina lake.
- Omba kwamba Roho Mtakatifu akupatie fursa maalum leo ya kushuhudia.
- Omba kwamba Roho Mtakatifu aongoze utume wa kanisa letu ulimwenguni kote.

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

### **Siku ya Pili – May 4**

#### **Unyenyekevu – Kuutafuta - Kugeuka**

*"Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao." – 2 Nyakati 7:14*

*Toba, unyenyekevu, roho iliyovunjika; Moyo uliovunjika na kupondeka, Mungu hataudharau*

#### **Changamoto ya Moyo.**

Dhambi ni mbaya sana na ya kutisha, kiasi kwamba hakuna kitu tunachoweza kufanya, hakuna kiasi cha mambo mema kinachoweza kuondoa makovu yaliyosababishwa na dhambi. Lakini Mungu katika rehema yake isiyokuwa na kikomo hatuambii kwamba tufanye kile tunachoweza kufanya wenywewe. Anakubali hali ya kujitoa kwa kawaida, kwenye unyenyekevu kwamba tunamhitaji. Je, unahisi kuhitaji msamaha wake? Uponyaji wake? Unaweza kuwa na huo uponyaji, tena leo hii! Unachotakiwa kufanya ni kumgeukia Yesu sasa hivi na kuomba huku ukiungama dhambi zako. Kisha chagua kuamini neema yake toshelevu ili ikuwezeshe kutembea kadiri unavyoupatia kisogo udhaifu na kugeukia haki yake.

#### **Mambo ya Kuombea**

- Omba kwamba Mungu akudhihirishie hitaji lako kuu la neama yake.

- Ombo kwamba Mungu akusaidie kuamini nguvu zake na kupata ushindi katika jitihada zako za kila siku dhidi ya dhambi.
- Ombo kwa ajili ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kwa mchungaji wa kanisa lako.
- Ombo kwamba Mungu arekebishe mahusiano yaliyovunjika katika Maisha yanayohitaji kurejeshwa na kukupatia moyo wa toba na unyenyekevu wa kweli ikiwa ulikuwa umewajeruhi wengine.

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:

<https://247unitedprayer.org>

### **Siku ya Tatu – May 5**

#### **Uamsho na Matengenezo – Uzoefu uliochanganyika.**

*“Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.”* – Ufunuo 3:20

*Uamsho na matengenezo ni lazima vifanyike, chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Uamsho na Matengenezo ni mambo mawili yaliyo tofauti. Uamsho unahusu badiliko la Maisha ya kiroho, kuhuishwa kwa nguvu, mawazo, na moyo, kufufuliwa kutoka katika kifo cha kiroho. Matengenezo maana yake ni kujipanga upya, badiliko la dhana na nadharia, tabia na mwenendo. Matengenezo yataleta tunda jema la haki ikiwa kutakuwa na muunganiko na uamsho wa Roho. Uamsho na matengenezo vinatakiwa kutenda kazi husika, na ili kufanya kazi hii lazima viwe vimeungajishwa.*  
– 1 SM, uk. 128

#### **Changamoto ya Moyo.**

Matengenezo ya Maisha yetu kuelekea katika mtu anayedhihirisha upendo wa Yesu ni kazi ya kutendeka Maisha yote. Kazi hii itafanya kadiri Roho Mtakatifu atakavyowezesha uhai ndani yetu. Nguvu za Mungu za uhuisho zinaleta uamsho kwetu na matokeo yake ni kuongezeka kwa njaa ya kuwa na Yesu. Lakini haiishii hapo. Uzuri wa uamsho ni kwamba ni zoezi endelevu na ni zoezi linaloongoza katika matengenezo ya kila Nyanja za Maisha yetu, kila fikira na kila mwenenedo.

Je, kuna wakati unapotamani kuwa na uamsho kuliko matengenezo? Unahofu kwamba ukisalimisha Imani, mpangilio wa mawazo, mazoea fulani, au mwenendo, kufanya hivyo kutakuondolea starehe fulani katika Maisha yako? Kwamba labda kufanya hivyo kutafanya Maisha yako yasiwe na msisimko?

Kumbuka kwamba Mungu huyo huyo unayemfahamu kama mwenye kusamehe, mwenye upendo, mwema, na Baba mwenye rehema, ndiye Mungu huyo huyo anayetamani kuleta matengenezo halisi kwenye Maisha yako. Je, utatumainia mapenzi yake leo? Je, utamkaribisha Yesu, siyo tu mlangoni pa moyo wako, bali aje ndani yako na kufanya makao yake ndani yako, akitumia muda pamoja na wewe, akikusaidia kupangilia upya Maisha yako, akirekebisha kila kitu upya moyoni mwako na kukarabati palipovunjika, akisafisha kila uchafu na vumbi na utandu ambaو dhambi imetengeneza.

### **Mambo ya Kuombea**

- Omba kwamba Mungu akupatie moyo ulio tayari kuishi kwa utii mkamilifu kwa mapenzi yake. Omba kwa ajili ya ushindi dhidi ya dhambi fulani maalum ambazo bado unapambana nazo.
- Omba kwa ajili ya vijana na waumini unaowafahamu ambaو wanaopambana na uraibu wa namna yoyote ile, mfadhaiko, au matatizo mengine yoyote ya afya ya akili.
- Ombea washiriki wa kanisa katika maeneo ya Ulaya Mashariki, kwamba Mungu aingilie kati na kutukuzwa katika janga hili la kuumiza linaloendelea.
- Omba kwa ajili ya waumini ambaو wanakabiliwa na mateso ya kidini sasa hivi, kama vile Asia na Mashariki ya Kati.
- Ombea ile orodha ya majina saba uliyo nayo.

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kuitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:  
<https://247unitedprayer.org>

### **Siku ya Nne – May 6 Ushuhuda wa Jerry Page**

#### **“Siku 40 za Maombi na Ndugu Yangu Alan”**

Na Jerry Page

Kaka yangu mkubwa kwa jina la Alan, alikuwa hashikiki akiwa mdogo, hadi akaishia kutengana na Bwana, na kuliacha kanisa sehemu kubwa ya Maisha yake. Hatimaye maisha yake ya ubinafsi yalimgharimu ndoa yake ya kwanza ilioishia kwenye talaka. Kazi yake ya huduma ya afya ilimpatia fedha nyingi, lakini aliipoteza fedha yote hiyo. Mara moja moja alijaribu kujihusisha na kanisa, lakini mtindo wake wa Maisha na mwenendo wake siku zote ulimvuta akarudi nyuma na kuzama tena katika Maisha bila Bwana. Familia yetu, pamoja na wazazi wetu wote tulimwombea Alan kwa miaka mingi ili akabidhi Maisha yake kwa Yesu.

Katikati ya mwaka 2010 mwanangu mdogo Zac aliyekuwa mchungaji na mke wake Lea, waliamua kumworodhesha Alan kati ya majina saba ya kujielekeza kwa maombi katika msisitizo wa siku 40 za maombi katika chuo kikuu cha Andrews. Wakati huo mimi pia nilisukumwa kwa namna isiyo ya kawaida kumsihi Mungu kwa ajili ya wokovu wake. Kwa namna ya ajabu tu mambo yalianza kutokea kwa jinsi ambayo Mungu aliruhusu katika mazingira ya maisha ya Alan.

Kiwewe kikubwa kilimkumba Alan. Mke wake wa pili alimkimbia, na ugonjwa wake wa kisukari ukawa mbaya zaidi, kiasi cha kumfaya akatwe mguu. Kila kitu kilionekana kumwendea kombo. Lakini siku moja akiwa amelala katika kitanda cha hospitali, hatimaye Alan alimfikia Yesu na kusema, "Ninatoa Maisha yangu yote kwako." Sote tulimtukuza Bwana.

Binti wake kwa jina la Christy alijitahidi kumsaidia baba yake kuanza kujenga upya mahusiano yake na Mungu na kanisa lake. Alipamba moto kuwashuhudia wengine na kugawa machapisho kwa muda. Lakini kama ujuavyo, majeshi ya Shetani hayachoki wala kukata tamaa kirahisi, na mara nyingine kuanguka na kuinuka, hatimaye akawa anajisikia kuwa hakustahili kutumika, na kwa hiyo akaacha safari yake ya kiroho tena.

Siku moja Alan aliniambia kwamba anadhani hawezi kufanya mabadiliko yaliyokuwa yanahitajika na kwa hiyo asingeweza kuishi na Bwana milele. Nilimshirikisha tena aya za Maandiko kuhusu uwezo wa Bwana wetu wa kuokoa, na nikamsihi asikate tamaa. Nilimwambia kuwa, "Familia yako haiwezi kukubaliana na hilo, tutaendelea kukuombea kwa nguvu zaidi. Yesu anaweza kukuokoa!"

Christy aliendelea kumpeleka katika kanisa dogo, na hapo walimwonesha upendo, naye akafurahia uhusiano wao. Alimshauri kuhudhuria kwenye semina za namna ya kupona ugonjwa wa kisukari. Alituambia kuwa ameondoa vyakula vyote kutoka kwenye jokofu alivyoziiliwa kama walivyosema, na hapakuwa na kitu kilichokuwa kimebaki.

Jioni moja ya Ijumaa, mwinjilisti wa kanisa mahalia alianzisha mfululizo wa masomo ya uinjilisti na hili kanisa dogo lilishiriki kikamilifu. Christy alimpeleka Alan kwenye mkutano wa kwanza usiku ule. Mwisho wake katika wito, huyu mwinjilisti aliwasihii watu waweke alama kwenye kadi zao kudhihirisha kwamba wangependa kuwa na Yesu mbinguni. Christy anasema Alan aliandika kujitoa kwake kwa maandishi makuba kuwa, "Nimejitoa na nimefunkwa na haki ya Yesu tena!"

Usiku ule Alan alikutwa amefia katika sakafu ya jiko lake kutokana na kupatwa na kiharusi. Ni Mungu wa ajabu tunayemtumikia. Alipata namna ya kumtumikia Mungu dakika za mwisho za Maisha yake. Alan alikuwa na umri wa miaka 75 alipofariki; familia yetu pamoja na wengine tulishirikiana kumwombea Maisha yake yote!

Je, umekuwa ukimwombe mtu fulani kwa miaka, na haujamwona akija kwa Yesu? Usije ukakata tamaa!

Nilipokuwa nikihudumu katika mazishi ya Alan nikisikiliza sifa za furaha za wake zake wawili aliotalkiana nao, mabindi wake wawili, na ndugu na jamaa wa karibu wengi, marafiki waliokuwa wakihuzunika, wafanya kazi wenzake, moyo wangu ulikuwa umejawa na furaha na sifa kwa Yesu kwa ajili ya uwezo wake wa kuokoa yeyote yule aliye tayari, wakati wowote! Wazazi wangu wapendwa walishafariki miaka mingi iliyopita kabla Alan hajamrudia Yesu. Litakuwa jambo la kushangaza kiasi gani asubuhi ile ya ufufuo watakapokuwa wakimkumbatia Alan na kuanza upya Pamoja na Yesu milele.

Ninawasihi kutumia hasa hizi siku 40 za maombi. Hebu fikiria kile ambacho Mungu wako asiye na mwisho anaweza kukufanya na kufanya kupitia kwako kadiri unavyoinua kwa dhati maombi yako kwake! Tunaambiwa kuwa, "Basi atukuzwe ye ye aezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu;" (Waefeso 3:20)

*Jerry Page ni Katibu wa Wachungaji wa Konferensi Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato.*

### **Changamoto ya Moyo.**

Je, kuma mtu fulani katika Maisha yako ambaye amegota katika kina cha giza? Au labda kuna mtu fulani unayemfahamu ambaye ametanga mbali kutoka kwa Mungu, au ambaye haonekani katu kujishikiza kwa Yesu? Kuna tumaini kwa mtu kama huyo, hata kama anaonekana kukata tamaa. Na sisi hatutakiwi kukata tamaa katika kuomba, kufanya maombezi, na kuhangaika kwa ajili ya wokovu wa hawa watu wa thamani.

Ni nani unayemuwazia kama mlengwa wa ushuhuda huu? Ni majina gani ambayo yanaweza kuhitaji kutajwa kila siku katika maombezi yako yasiyokoma?

### **Mambo ya Kuombea**

- Omba kwamba Mungu akufundishe jinsi ya kuunganisha ufa uliopo kwa wale wenye uhitaji ndani ya siku hizi 40 za maombi.
- Omba kwa ajili ya ile orodha ya watu 7 maalum na kuomba kuhusu mahitaji fulani maalum unayofahamu.
- Omba kwa ajili ya majaliwa kwa wale ambao hivi karibuni wamepoteza miji yao au hata wapendwa wao kwa moto, mafuriko, magonjwa au majanga mengine yoyote ya asili.
- Waombee wamisionari unaowafahamu, ambao wako mbali na nyumbani kwao au mbali na familia zao ili kwamba wajazwe na furaha katika huduma yao.

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:  
<https://247unitedprayer.org>

### **Siku ya Tano – May 7**

### **Sabato ya Mambo ya Kuombea**

- Omba kwa ajili ya mibaraka maalum ya Sabato leo, na kwamba Mungu azungumze nawe kwa namna binafsi.
- Ombea ile orodha ya watu 7 uliowachagua.
- Ombea majirani zako ambao hawamfahamu Mungu
- Omba kwa ajili ya watendakazi katika shamba la Mungu ambao wamejazwa na Roho Mtakatifu na kuwa na ari ya kujitoa kikamilifu.
- Ombea namna Mungu anavyoweza kukutuma katika kazi mahususi kwenye huduma yake.

### **Siku ya Sita – May 8**

### **Jumapili ya Mambo ya Kuombea**

- Ombea mukutano mkuu wa Konferensi kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato utakaofanyika St. Louis, Marekani tarehe 6 hadi 11 June 2022
- Omba kwa ajili ya fursa binafsi za kuwaelekeza wanafunzi na kuwafanya washiriki wapya kuwa wanafunzi.
- Ombea mapenzi ya Mungu kwa uchaguzi unaokuja na uteuzi wa viongozi wapya.
- Ombea chumba cha maombi kilicho katika eneo husika kwa ajili ya mukutano mkuu wa Konferensi Kuu, na vyumba vyaya kimtandao vyote vilivyopo pamoja na wote watakaohudhuria.
- Ombea ile orodha ya majina ya watu wale saba uliowachagua.

**Vyanzo vingine vya kukusaidia kuzama kwa kina.**

[Experiencing God through Prayer and Praise, Principles of Intercessory Prayer, and More – Collection by Jerry and Janet Page](#)

**Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:  
<https://247unitedprayer.org>

**Juma la 2: Mei 9 – 15**

**Siku ya Saba – May 9 – Wazo la Kesha: Utume – Jihusishe**

### **“Utume - Jihusishe”**

Na Ted N. C. Wilson

Tunaishi nyakati za mabadiliko yasiyokuwa na mfano. Mungu anawaita watu wake masalia, ambao ni Waadventista wa Sabato, kuandaa njia ya Bwana wakimtegemea kikamilifu, ili kupokea nguvu ya mvua ya masika ya Roho Mtakatifu, na kujihusisha katika utume wake. Hatimaye ni wakati wa kilio kikuu... kutangaza ujumbe wa Malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Kristo ametuita kuwa wapanzi wa Neno na kuhusika kikamilifu katika utume wa Mungu wa mwisho wa kutangaza ujumbe wa Kristo wa Malaika watatu. Kila mmoja wetu anaitwa kuingia ubia na Mpanzi wa mbinguni, ambaye ni Yesu Kristo ili kushiriki katika utume wa kanisa wa kutangaza ujumbe wa mwisho wa Mungu wa upendo, haki, ukombozi, na ujumbe wa maonyo wa kiunabii wa siku za mwisho unaotangaza kurudi kwa Yesu ambako kumekaribia. Kila mmoja ni mpanzi... kila mmoja anayehusika katika utume! Kila mmoja anayesema kuwa, “Naam Bwana Nitakwenda kutangaza Neno lako!” Kuwahuhsisha Washiriki Wote maana yake

ni kwamba kila mmoja anatakiwa kufanya kitu fulani kwa Bwana! Kama vile Neno Kuu la Mkutano Mkuu wa Konferensi Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato lisemavyo kuwa, "Yesu Anakuja! Jihusishe!"

Kitabu cha Marko sura ya 4 kinamwonesha Yesu akizungumza na maelfu katika bahari ya Galilaya. Wasikilizaji waliweza kuona uwanda mpana, vilima ng'ambo ya wapanzi na wavunaji ambao walikuwa wameshikika katika kumwaga mbegu na kuhakikisha kila punje ya nafaka inavunwa.

Tunasoma katika Marko 4:3-9 kuwa, "Sikilizeni; Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda; ikawa alipokuwa akipanda, mbegu nyingine ilianguka kando ya njia, wakaja ndege wakaila. Nyingine ikaanguka penye mwamba, pasipokuwa na udongo mwingi; mara ikaota kwa kuwa na udongo haba; hata jua lilipozuka iliungua, na kwa kuwa haina mizizi ikanyauka. Nyingine ikaanguka penye miiba; ile miiba ikamea ikaisonga, isizae matunda. Nyingine zikaanguka penye udongo ulio mzuri, zikazaa matunda, zikimea na kukua, na kuzaa, moja thelathini, moja sitini, na moja mia. Akasema, Aliye na masikio ya kusikilia, na asikie."

Marko 4:14 panasema kuwa, "Mpanzi huyo hulipanda neno." Mathayo 13:37 panaonesha kwamba mpanzi wa mbegu njema ni Mwana wa Adam, yaani Yesu Kristo. Tunatakiwa kuingia ubia naye kwa kujihusisha kwenye utume wake kama wapanzi wa ukweli. Kitabu cha "Christ Object Lesson" ukurasa wa 36 panasema kuwa, "Watumishi wake lazima waendelee kupanda kwa jinsi hiyo hiyo." Kila mmoja anatakiwa kujihusisha katika utume wa kupanda Neno la Mungu lililo takatifu la Kuwahusisha Washiriki Wote katika siku hizi za mwisho wa historia ya dunia hii.

Fungu la 15 linasema kuwa, "Hawa ndio walio kando ya njia lipandwapo neno; nao, wakiisha kusikia, mara huja Shetani, akaliondoa lile neno lililopandwa mioyoni mwao." Neno la Mungu la thamani linaanguka kwa wasikilizaji wenye usikivu kama mapito yasiyokuwa na kina.

Mafungu ya 16-17 yanasema kuwa, "Kadhalika na hawa ndio wapandwao penye miamba, ambao kwamba wakiisha kulisikia lile neno, mara hulipokea kwa furaha; ila hawana mizizi ndani yao, bali hudumu muda mchache; kisha ikitokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara hujikwaa." Mbegu hizi haziwezi kupata udongo mzuri ili zikue. Kwa sababu mizizi haiwezi kuzama ndani ya udongo wa mawasiliano na Kristo kila siku, mateso na majaribu yanashika hatamu. Kile kitabu cha 'Christ's Object Lesson, uk. 48 tunasoma kuwa, "Wengi watapata hisia za kutengwa kutoka kwa Mungu, kutambua uteja wao kwa ubinafsi na dhambi; wanatafuta namna ya kubadilika; lakini

hawaisulubishi nafsi.” Kaa karibu na Mungu na ukijizuia kuwa msikivu wa “udongo wenyewe mwamba”

Mafungu ya 18-19 “Na hawa ndio wale wapandwao penye miiba; ni watu waliskiao lile neno, na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali, na tamaa za mambo mengine zikiingia, hulisonga lile neno, likawa halizai.” Katika ‘Christ’s Object Lesson, uk. 50 tunasoma kuwa, “Neema inaweza kudumu tu katika moyo ulioandaliwa kwa ajili ya mbegu za thamani za ukweli.” Kaa karibu na Bwana kuititia katika kujifunza Biblia, Roho ya Unabii na maombi ya kudumu

Fungu la 20 tunasoma kuwa, “Na hawa ndio waliopandwa penye udongo ulio mzuri; ni watu waliskiao lile neno na kulipokea, na kuzaa matunda, mmoja thelathini, mmoja sitini, na mmoja mia.”

Mungu amekusudia kwamba sisi sote tuwe “udongo mzuri kwa wasikilizaji” ambao wanatumaini kikamilifu katika haki ya Kristo na kusema, “Bwana, Nitakwenda” kupanda Neno lako. Kila mmoja lazima ajihusishe katika utume mkuu wa mwisho wa Mungu wa maonyo na matumaini. “Yesu Anakuja! Jihusishe!”

*Ted N. C. Wilson ni Mwenyekiti wa Konferensi Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato*

### **Changamoto ya Moyo.**

Kila hubiri tunalosikia, kila andiko tunalosoma, Mungu anapanda mbegu. Mara nyingi inatia ujasiri, na wakati mwingine inaleta changamoto, lakini tunaweza kuwa na uhakika kwamba, Neno la Mungu lenye uwezo litafanya kile lililokusudiwa kufanya ndani ya mioyo yetu na katika Maisha yetu ikiwa tutamruhusu, maana yake kama tutapokea Neno, kulitafakari, kulitunza, na kilitenda.

Kusudi la kupokea Neno la Mungu na kuliruhusu kubadilisha Maisha yetu ni ili tuweze kushiriki ujumbe wa Habari njema na watu wanaotuzunguka. Mpanzi kutoka mbinguni ametufanya sisi kuwa wenzake katika zoezi la kupanda pamoja naye. Je, utafungua moyo wako kupokea mbegu zake leo? Utajiunga katika utume wake kushiriki mbegu zake na yejote anayeletwa mbele ya mapito yako?

### **Mambo ya Kuombea**

- Ombe ili kupata uelewa wa Neno la Mungu na kuweza kufungua moyo ili Neno lipate kuumba Imani yako na thamani yako
- Ombea ndugu zako na dada zako waliopo Shanghai, China
- Ombea ujasiri wa washiriki wa kanisa letu kule Urusi na Ukraine.

- Ombea magazeti na vitabu vya Watoto ambavyo vimeandikwa hivi karibuni mahususi kwa ajili ya watu wa Ukraine, kwamba hivi vyanzo maalum viwafikie kwa wakati na kuleta miyo mingi katika ufalme.
- Omba kwamba wito wa “Yesu Anakuja! Jihusishe!” uwe na kipaumbele chenye umuhimu katika Maisha yako ya kila siku.

### **Vyanzo vingine vya kukusaidia kuzama kwa kina.**

[How to Be Part of Total Member Involvement](#)

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:  
<https://247unitedprayer.org>

## **Siku ya Nane – May 10**

### **Ninyi ni Nuru**

*“Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.” – Mathayo 5:14-16*

*Ubinadamu wenyewe hauna nuru. Kando ya Kristo sisi ni kama mshumaa uliozimwa, ... Lakini tunapoligeukia Jua la Haki, tumapogusana na Kristo, nafsi yote inaangazwa kwa mng’ao wa uwepo wa mbingu. Wafuasi wa Kristo wanatakiwa kuwa zaidi ya nuru kati ya wanadamu, wao ni nuru ya ulimwengu... Malaika wa utukufu wanashubiri kuwasilisha kupitia kwenu nuru ya mbinguni na nguvu kwa roho zilizo tayari kuangamia - Thoughts From the Mount of Blessing, uk. 40*

### **Changamoto ya Moyo.**

Je, umesoma nukuu hiyo hapo juu? Pengine urudie kuisoma tena. Je, unatambua kwamba Malaika wanashubiri kufanya kazi kupitia kwako ili kuwafikia watu waliopotea? Hilo si ni jambo la kushangaza?

Unakaribishwa siyo tu kujazwa na Roho Mtakatifu kwa ajili ya utakaso wako wewe mwenyewe, bali pia ili ushiriki kwa namna iliyo hai katika kupeleka ukweli, upendo, na haki ya Yesu kwa ulimwengu ambao muda wake umeisha.

Fikiria kuhusu familia yako, marafiki zako, majirani zako, wafanyakazi wenzako. Mwombe Mungu akuoneshe ni yupi anahitaji nuru ya Yesu katika maisha yake. Akuoneshe kuwa ni yupi unayepaswa kumwombea na hasa kumfikia juma hili.

### **Mambo ya Kuombea**

- Omba kwa dhati kwa ajili ya yale majina ya watu 7 waliopo katika orodha yako.
- Mwombe Mungu akusaidie kuona haja za watu unaowaombea na akupatie hekima ya namna ya kuwasaidia.
- Ombea taasisi za matibabu ya Kiadventista katika maeneo yako, na kote ulimwenguni, ili ziwe nuru kwa utukufu wake katika kuwafikia wale ambao wanahitaji uponyaji na kutiwa moyo.
- Ombea waumini wanaopambana huko Sudan kadiri hali ya uchumi inavyoyumba na ukame kusababisha bei za vitu kupanda wakati huo huo ukipunguza mazao.
- Omba kwamba Mungu avunje minyororo inayowafunga wengi katika utumwa wa kiroho

### **Junge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Junge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

### **Siku ya Tisa – May 11**

#### **Kuifikia Familia Yako**

*“Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini.”* – 1 Timotheo 5:8

*“... ni lazima uwe mkweli, imara, na uliyeamua kutimiza wajibu wako katika familia yako, na kuandamana nao ikiwezekana. Usipuuze jitihada yoyote ya kuhakikisha wanaandamana nawe katika safari hii ya kuelekea mbinguni.”* The Adventist Home, p. 352

#### **Changamoto ya Moyo.**

Sisi sote tunao ndugu na jamaa ambao bado hawajaingia katika upendo na Yesu wala hawajaamua kuishi kwa uaminifu kwa ajili yake. Au pengine kuna wakati walimfuata Yesu lakini sasa wametanga mbali. Inawezekana pia kwamba baadhi yao hawamwamini Mungu au wana sababu nyingine tu kwa ajili ya maamuzi yao. Au, labda hawajawahi

kupata fursa ya kusikiliza kwa ukamilifu, kuelewa na kuona injili kwa maneno na kwa matendo.

Una wajibu wa kufanya kwa kadiri ya uwezo wako kuwafikia hao wana-familia kwa upendo, upole, wema na hekima nyingi ukiwaonesha kwamba unajali, na kwa wakati muafaka kuwaelekeza katika ukweli na upendo wa Yesu.

Je, utafanya kazi hii iliyo muhimu ya upatanisho na huduma kwa maombi kwa ajili ya hawa wanafamilia wasiomwamini Mungu na wale wasio Waadventista wa Sabato? Utajitoa kwa dhati na kukusudia kutoka na kuwafikia?

### **Mambo ya Kuombea**

- Ombea familia yako. Je, kuna baadhi ya wana-familia unaohangaika nao? Waombee hao mahususi, na pia jiombee kadiri unavyotafuta namna ya kuwahudumia, ukiwalekeza kwa Yesu kupitia kwa maneno na matendo.
- Waombee washiriki wa kanisa lako na kusanyiko lenu kwa ujumla wale waliorudi nyuma
- Omba kwamba Mungu awapatie Watoto wako (au Watoto wako wa kiroho) nguvu za kuweza kusimama dhidi ya mashambulizi na udanganyifu wa Shetani. Dai Isaya 49:25 kadiri uanvyoomba.
- Omba kwa ajili ya usalama na kuhifadhiwa kwa Imani ya Watoto wako. Omba kwamba washike moto wa kujihusisha katika utume binafsi.
- Omba kwamba Roho wa Mungu amwagwe kwa nguvu juu ya wanafamilia na kila kiongozi na hata wafanyakazi wa Konferensi Kuu

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulmwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

### **Siku ya Kumi – May 12**

#### **Kuufikia Mji Wako**

*“Kautakieni amani mji ule, ambao nimewafanya mchukuliwe mateka, mkauombee kwa Bwana; kwa maana katika amani yake mji huo ninyi mtapata amani..”* – Yeremia 29:7

*"Umuhimu wa kuelekea kwenye miji mikuu uliendelea kuwekwa wazi mbele yangu. Kwa miaka mingi Bwana amekuwa akitusisitizia wajibu huu, lakini bado tunaona mafanikio madogo sana katika vituo vikuu vya wingi wa watu kwa kulinganisha. Ikiwa hatutaingia katika kazi hii kwa kudhamiria na kwa dhati, Shetani atazidisha magumu kiasi kwamba itakuwa vigumu kuvuka na kushinda. Tuko nyuma sana katika kufanya kazi ambayo ingekuwa imeshakamilika katika miji hii iliyopuuzwa kwa muda mrefu. Sasa hivi kazi itakuwa ngumu zaidi kuliko jinsi ambavyo ingekuwa miaka michache iliyopita. Lakini tukiingia katika kazi hii kwa Jina la Bwana wetu Yesu, vikwazo vitaondolewa, na ushindi wa dhati utakuwa ni wa kwtetu."* Ministry to the Cities, uk. 25

### **Changamoto ya Moyo.**

Sehemu kubwa ya wingi wa watu inaishi mijini. Wakati tukiendelea kumuliza Mungu wakati muafaka wa kuhama kutoka mijini, tunatakiwa pia kutokupuuza kazi katika hiyo miji. Mabilioni wamenasa bila tumaini katika uraibu, kelele, ukengeufu, na mitindo ya Maisha katika miji.

Mwombe Mungu aweke juu yako mzigo wa huduma katika miji. Pengine anakuita uanze "kituo cha mvuto" au biashara yenye mwelekeo wa huduma ili kuzifikia roho zilizopotea katika miji ya ulimwengu huu? Au labda anakuita wewe pamoja na kanisa lako uingie katika ujumla wa kuwafikia watu wa mji wako kupitia huduma mbali mbali?

Kwa nini usimwombe Mungu akuoneshe namna bora ya kuwahudumia watu wa mji au Kijiji chako?

### **Mambo ya Kuombea**

- Omba kwa ajili ya ustawi wa mji wako mwenyewe. Omba kwamba injili iangaze kwa mng'ao kupitia kwako na kwa kanisa lako katika mji wako.
- Omba kwa ajili ya meya wa jiji/mji/Kijiji chako, na kwa viongozi wa jumuia zingine. Omba kwa ajili ya wokovu wao na pia ili Mungu awapatie hekima kwa ajili ya uongozi mwema.
- Ombea miji isiyokuwa na uwepo wa Waadventista wa Sabato – kwamba Mungu ainue watendakazi kwa ajili ya mavuno.
- Omba kwa ajili ya vituo vya mijini duniani kote, utume kwa miji na vituo vya mvuto vilivyo katika maeneo ambayo hayajafikiwa ulimwenguni kote. Omba kwamba watu wengi waletwe kwa Yesu.
- Omba kwa ajili ya uongozi katika vituo hivi, ili wapate hekima ya kutekeleza utume wao kwa kuendeleza Ufalme wa Mungu.

**Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

## **Siku ya Kumi na Moja – May 13 Ushuhuda wa Sebastien Braxton**

### **“Kunukia Kama Malaika”**

Na Sebastien Braxton

Nilipogonga mlango tu, mwanamke mwenye umri wa makamo akiwa na mwili mdogo hivi, aliufungua kidogo na kunisalimu. Nilianza kueleza kwamba nilikuwa ninapita nyumba kwa nyumna nikiuza machapisho ya Kikristo. Alikatiza haraka na kuniomba nije kesho yake. Alionekana kama aliyekuwa na msongo hivi. Nilimjibu nikijenga katika uzoefu wangu kwamba, “Mama, kwa uzoefu mara nyingi huwa haturudi. Kwa hiyo ikiwa haujisikii, ni vyema tu. Hata hivyo nina mfano wa vitabu ninavyoweza kukupatia kwa dola kumi hadi ishirini tu...” Hata hivyo alipuuza kauli yangu na kuniomba nirudi siku inayofuata. Nilikubaliana naye shingo upande na kuahidi kurudi. Mlango ukafungwa kwa nguvu.

Pamoja na ubishi wangu kwa ushawishi wa Roho, nilirudi tena nyumbani hapo. Kabla sijamaliza kupiga hodi, mlangu ulifunguliwa, na akanikaribisha ndani nimsubiri akiwa jikoni. Nilishawishika kwamba pengine nilikuwa ninapoteza muda wangu tu, na kwamba sikuwa nimebeba vitabu vyote. Nikaanza kujuta kwa uamuzi huo. Nikiwa nimekaa, mbele yangu kulikuwa na cheki juu ya meza ikiwa imeshasainiwa. Kwa haraka nilichukulia kwamba alikuwa tayari kununua vitabu, na kuwa labda alikuwa anahitaji tu kufahamu bei. Nilianza kuungama kwa yule Roho aliyenishurutisha kuja, kwa sababu ya ukosefu wangu wa Imani. Yule mama aliporudi alikuta nimepanga vitabu mezani naye akasema kuwa, “Nitanunua vitabu vyote ulivyo navyo ikiwa utanijibu swal moja.” Kwa mshtuko nilisema kuwa, “Naam, kila kitu!”

Aliuliza kuwa, “Je, wewe ni Malaika?”

Nikaashiria kukataa kwa kichwa, nikiongezea “Hapana mama, mimi siyo Malaika.”

“Una uhakika wewe siye Malaika?” aliuliza akiwa na mashaka

"Ndiyo, nina uhakika. Unaweza kumuuliza mama yangu, atakuambia." Nilimwambia kwa mguno kidogo. Kisha nikamuuliza kwa udadisi, "Kwa nini uniuilize hivyo?"

Jibu lake lilibadilisha uelewa wangu wote kuhusu namna Mungu alivohusika kutuunganisha. Yule mwanamke aliniambia kwamba mwaka mmoja uliopita aliota akizungumza na Malaika, lakini hakuweza kuona uso wake kwa sababu ya mng'ao wa huo uso. Alipoamka akidhani kuwa ni ndoto, alikaa na kutambua kwamba haikuwa ndoto, yule Malaika alikuwa mwisho wa kitanda chake upande wa miguuni. Ndipo yule Malaika akapaa taratibu kupitia dirishani, na kwa haraka huyo mama akakimbilia dirishani ili apate kumwona vizuri – lakini hakumwona.

Alivyojirudisha kutoka dirishani, kukawa na manukato mazito chumbani. Hayo manukato yalikuwa yakinukia vizuri kwa namna isiyo ya kawaida. Alianza kuchunguza mahali hayo manukato yanapotokea. Alinusa kila uturi aliokuwa nao hapo ndani: cologne, herb, essence, kila aina aliyodhani. Hakuna iliyofanana kwa kunukia hadi jana nilipojitekeza mlangoni pake. Huyu mwanamke akaniambia, "Jana ulikuwa na hayo manukato! Nilishtuka sana kiasi kwamba niliingiwa na hofu, ndipo nikakuomba urudi asubuhi ya leo. Nilifikiria kuwa, ikiwa wewe ni Malaika kutoka kwa Mungu, utarudi na kwamba Malaika hawezi kusema uongo."

Ni kweli kidogo nisirudi! Ningekosa fursa ya kuwa sehemu ya muujiza wa Mungu kwa kukata tamaa kwa ajili ya roho ninazokutana nazo katika huduma.

Basi huyo mama aliendelea kusema kuwa, "Hata sasa bado unanukia yale manukato." Tuliomba pamoja na kukumbatiana, na akaomba apewe masomo ya Biblia.

Kama vile uzoefu wa Kornelio wa leo katika kitabu cha Matendo sura ya 10, Mungu anaandaa mtu fulani sasa hivi kwa ajili yako. Ninaamini Mungu alibakiza ile harufu ya manukato kwa mwaka mzima ndani ya yule mama ili kuthibitisha mamlaka ya kimbingu kwa yejote atakaye kuwa na harufu hiyo tena. Nashukuru kuwa Mungu hamwangalii mtu, bali kwa furaha atampatie uzoefu huo huo yejote aliye tayari kujitoa kwa ajili ya wokovu wa wengine. Ikiwa uko tayari kujitoa kwa uongozi wa Roho Mtakatifu na kujikabidhi kwa mbingu, ndipo na wewe utakuwa unanukia "manukato kama Malaika" kwa zile roho ambazo Mungu ameziandaa kupokea neema yake na wokovu wake.

*Sebastian Braxton ni msanifu wa UX, mzungumzaji wa kimataifa na mjasiriamali wa mlolongo. Yeye ni Mtendaji Mkuu na mwanzilishi wa "Luminate" ambao ni mfumo wa mtandao unaosaidia uzoefu wa sauti kupitia maandiko ya Ellen G. White. Yeye ni mwanzilishi wa "Fiat Lux" ambao*

*ni wakala wa ubunifu ambao unatoa maoni kwa mashirika ya kidini kwa kutegemeza teknolojia kwa injili.*

### **Changamoto ya Moyo.**

Tunapokuwa tayari kutumiwa na Mungu, yeye ataongoza uteuzi wa kimbingu ambao siyo tu kwamba una mibaraka kwa wale watu tunaowahudumia, bali pia mibaraka hiyo itatutia moyo katika kutembea kwetu na Kristo. Hakuna kitu cha kusisimua kama kutembea na Yesu na kufahamu kwamba anafanya kazi kwa niaba yetu kadiri tunavyojiunganisha naye katika kazi yake.

Je, ni lini kwa mara ya mwisho ulipoomba ili Mungu akufanyie uteuzi wa kimbingu? Kwa nini usisalimishe muda wako, hofu zako, na wewe mwenyewe, kwa Kristo sasa hivi, na kumwomba Mungu akutumie kumfikia mtu fulani kwa ajili yake?

### **Mambo ya Kuombea**

- Omba kwa ajili ya uteuzi mahususi wa kimbingu leo na mwisho wa juma hili.
- Omba kwamba Mungu akupatie watu utakaojifunza nao masomo ya Biblia na uondoe hofu yoyote uliyo nayo moyoni ya kujifunza na wengine
- Omba kwa ajili ya ndugu zako na dada zako walioko China, ambao wanapambana chini ya mateso ya kidini.
- Ombea waumini walioathirika na mafuriko kule Durban, Afrika Kusini na Ufilipino.
- Ombea yale majina ya watu saba kwenye orodha yako. Omba upate namna ya kuwafikia.

## **Siku ya Kumi na Mbili – May 14**

### **Sabato ya Mambo ya Kuombea**

- Omba kwa ajili ya hekima kwa viongozi wa kanisa katika mukutano mkuu wa Konferensi Kuu kule St. Louis, Markani tarehe 5 hadi 11, 2022
- Omba kwa ajili ya watu wa Ukraine na hasa kwa washiriki wa kanisa katika maeneo yaliyoathirika kwa mgogoro huo. Omba kwamba wao wawe ni nuru angavu kwa watu wanaoumia katika maeneo yao.

- Omba kwa ajili ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kwenye huduma ya machapisho ulimwenguni kote. Omba kwamba huo uwe ni mlango ambao utawaongoza wengi katika kumkubali Yesu Kristo.
- Omba kwa ajili ya watu wa Afghan waliolazimishwa kuwa wakimbizi
- Omba kwamba Mungu aingilie kati katika kuongezeka na kupaa kwa bei za mafuta ya magari na vyakula, hasa kule Peru mahali ambapo kumetamkwa hali ya hatari. Omba kwamba Mungu akutane na mahitaji ya watu wake sawa sawa na utajiri na utukufu wake.

## **Siku ya Kumi na Tatu – May 15**

### **Jumapili ya Mambo ya Kuombea**

- Ombea yale majina 7 ya watu waliopo kwenye orodha yako.
- Waombee wale ambao waliooneshwa kujali na lile tuko la “Mapito kuelekea katika Afya” la mwezi wa April kule Indianapolis. Omba ili mbegu zipate mizizi.
- Omba kwamba Mungu aandae viongozi wa kanisa lake kwa ajili ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu.
- Ombea kile chumba cha maombi kilichoko katika Konferensi Kuu kwa majira yake ili wengi wabarikiwe, na kwamba majibu yapatikane wote wapate uamsho wa pekee wanapokuja kwenye maombi.
- Omba kwa ajili ya maombi ya saa 24 kwenye chumba cha maombi ambapo wengi tayari wanakutana kwa mtandao katika siku hizi 40 za maombi. Pitia kwenye tovuti hii: <https://247unitedprayer.org>

**Vyanzo vingine vya kukusaidia kuzama kwa kina.**

[Here's Your Church Back – Message by Sebastien Braxton](#)

**Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

**Juma la 3: Mei 16 – 22**

**Siku ya Kumi na Nne – May 16 – Wazo la Kesha: Utume – Neno**

## **“Nguvu ya Neno”**

Na Sikhu Daco

Ilikuwa ni siku nzima ya huduma ya kuhubiri, na Yesu alikuwa amechoka. Hadhira yake haikutambua hilo, lakini Yule aliyeongea nao siku hiyo alikuwa ndiye Neno lililoumba vitu vyote hapo mwanzo. Hata hivyo nguvu ya Neno ingeweza kuzamishwa ndani ya Maisha ya wale ambao wamechagua kuweka Imani yao katika uzoefu ndani ya Yeye atoae uzima. Jemedari wa majeshi ya mbinguni, sasa akiwa amechoka kutokana na kazi yake, aliwaagiza wanafunzi wake kuvuka ng'ambo ya ziwa. “Wakauacha mkutano, wakamchukua vile vile alivyo katika chombo. Na vyombo vingine vilikuwako pamoja naye.” (Marko 4:36)

Ghafla Dhoruba ikaanza wakati mitume walikuwa katika kuvuka. Pamoja na uzoefu wao wa mashaka ya majini, hawakuweza kumudu hali yao. Kwa jitihada zote walizofanya, hekima ya kibinadamu ilifikia kikomo, na hatimaye waligundua kwamba Yesu alikuwa ndani ya chombo pamoja nao, ndipo wakamlilia wakisema, “Bwana, tuokoe, tunaangamia.” (Mathayo 8:21)

Ilikuwa ni kwa amri ya Yesu kwa zile pepo kwamba waliweza kuendelea majini hadi ng'ambo ya ziwa, lakini hata hivyo ni kama walionekana kusahau kwamba Yesu alikuwa pamoja nao ndani ya chombo. Walijikuta kwenye Dhoruba kwa sababu walikuwa wamechagua kutii amri ya Yesu Kristo, lakini mwenendo wao ulikuwa kama vile ilikuwa ni jukumu lao wenyewe kuhakikisha utekelezaji wa agizo lile. Wakiwa wameanza safari pamoja na Kristo, kwa kutii Neno lake, sasa waligeukia uwezo wa kibinadamu kutafuta kutekeleza kile ambacho Neno lake lilikuwa limeamuru.

Katika kuitikia Neno la Mungu likizungumza katika Maisha yatu, wengi wameanza safari yao ya Kikristo. Lakini Mungu hakukusudia iwe hivyo. “Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye;” (Wakolosai 2:6). Uwezo wa kutegemeza uzoefu wa Ukristo wetu ni uwezo huo huo unaotubadilisha, na umejikita katika Neno la Mungu. Wanafunzi wa Yesu wangeweza kupushwa mashaka mengi kama wangekumbuka kwamba, ikiwa Neno lake limemkuagiza au limekuamuru, ni Neno hilo hilo litakalokutegemeza.

Yesu akiamka kutoka katika usingizi wake mzuri kati kati ya Dhoruba kuu, alitamka, "akaukemea upepo, akaiambia bahari, Nyamaza, utulie. Upepo ukakoma, kukawa shwari kuu" (Marko 4:20). Ni dhahiri kwamba vitu vya asili vilitii Neno lake! Kama asingekuwa amekemea mapepo (Marko 1:23-27), kama asingekuwa ameponya wagonjwa (Marko 1:30-34; 2:3-12; 3:1-5), na ameponya wenyewe ukoma (Marko 1:40-42)? Kama wanafunzi wake wasingeshangazwa na mafundisho yake: "Wakashangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi." (Marko 1:22). Lakini hawakutambua jinsi Neno lake lilivyokuwa na nguvu.

Yesu alipozungumza, Neno lake liliumba uhalisia. Yale yote aliyoamuru kwa Neno lake, ni kweli kwamba anaahidi kutekeleza katika Maisha ya wale wote ambao wataweka Imani yao kwake katika utendaji. Kwa hiyo inasemekana kuwa, "Kadiri ambavyo nia ya mwanadamu inashirikiana na mapenzi ya Mungu, inakuwa yenyewe kudura. Lolote litakalofanywa kufuatia agizo au amri yake, linaweza pia kufanyika na kwa nguvu yake. Maagizo yake yote yanawezesha." (Christ's Object Lesson, uk. 331-333). Kinachobakia kwetu ni kuamua kama tutaruhusu Neno lake lifanye kazi yake katika Maisha yetu.

*Sikhu Daco ni mjumbe wa jopo la onesho la Hope Channel TV linaloitwa "InVerse" ambalo linajadili mwongozo wa kujifunza Biblia kwa jina hilo hilo. Yeye ana digrii ya uzamili katika Elimu kutoka Seminari ya Teolojia ya Chuo Kikuu cha Andrews*

### **Changamoto ya Moyo.**

Kama sisi wanadamu kwa namna ya asili tu tunaamini katika dhana zetu binafsi na mtazamo wa kidunia kabla ya kuchukulia taarifa za nje. Kiburi kinaweza kutuongaoza katika kushindwa kuona na kusikia taarifa husika ambazo zinaweza kutubadilisha. Lakini tunaposalimisha Maisha yetu kwa Yesu, Roho atatuongoza katika kuhoji dhana zetu wenyewe, mawazo, na Imani zetu kwa kuziangazia nuru ya ukweli wa Mungu kama unavyodhihirishwa katika Neno lake. Ufunguo mmoja muhimu wa ukuaji wa kiroho ni kuruhusu nuru yake kutuangazia na kuongoza mapito yetu kwa kutenga muda wa kutosha katika kusoma na kujifunza, na kuomba kupitia katika Neno lake ambalo ni Biblia.

Ni lini ambapo kwa mara ya mwisho ultienga muda usiokuwa na haraka wala kuingiliwa wa kuzamisha Neno la Mungu na kuruhusu ukweli usio wa kawaida kuleta mng'ao katika Maisha yako?

Kwa nini usipunguze muda unaotumia katika mambo yako mengine, na kuuelekeza katika mafunzo ya kina ya Biblia. Haijalishi kiasi gani unachosoma na kujifunza.

Umuhimu upo katika kutafuna kwa ukweli aya au kisa hadi uwezo wake wa kubadilisha maisha, na kanuni ziletazo nuru ziwe zimebinafsishwa na kuwa tayari kuwekwa katika utendaji.

### **Mambo ya Kuombea**

- Ombe aushindi dhidi ya mivuto ya kidijitali katika simu au kompyuta inayokuondoa katika usikivu.
- Omba kwamba uongozwe dhidi ya mivuto iliyo hatari ya uchawi ambayo mara nyingi inamiminika kupitia katika mitandao ya kijamii.
- Omba kwa ajili ya familia ya kanisa la ulimwengu, ili wawe na nguvu kwa uwezo wa Mungu kuvunja vunja ngome za uraibu, mivuto na mahangaiko mengine yote ili tuweze kuwa ni jeshi lililo imara ambalo Mungu ameahidi.
- Ombea hekima ya namna ya kufanya ibada binafsi ya kila siku iwe ni kipaumbele.
- Ombea majina ya wale watu 7 uliowaorodhesha, kwamba hawa watu wagundue ushindi na furaha ya muda wa kuwa na Yesu.

**Vyanzo vingine vya kukusaidia kuzama kwa kina.**

[Unplugged: Disconnect to Reconnect by Frank Hasel](#)

**Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:  
<https://247unitedprayer.org>

### **Siku ya Kumi na Tano - May 17**

#### **Neno - Upanga**

*"Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."* – Waembrania 4:12

*Unaweza kujifunza Biblia kwa namna yoyote ambayo ungejifunza kitengo cha sayansi, lakini uzuri wake ambaa ni udhihirisho wa nguvu zake za kuokoa roho zinazoamini, ni fundisho ambalo hatujajifunza bado. Ikiwa utendaji wa Neno hautawekwa maishani, ndipo upanga wa roho utakuwa umeshindwa kujeruhi moyo wa asili. Imefunikwa na ushairi usiokuwa dhahiri. Mhemuko*

*wa hali ya juu umeisitiri kiasi kwamba moyo haujapata hisia kamilifu za wema wake, uchomao na kukatilia mbali mng'ao wa dhambi mahali ambapo ubinafsi unaabudiwa.*

### **Changamoto ya Moyo.**

Biblia imeja matumaini. Ina kila kitu tunachohitaji. Habari njema ya wokovu imewasilishwa kwa namna iliyo dhahiri kwa msomaji. Lakini vitu vyote hivi vya asili vilivyo vya ajabu havina maana kama havihami kutoka katika fikira zetu hadi miyoni mwetu hadi kwenye matendo yetu. Kushikilia ahadi zilizopo katika Neno kunakuwezesha kuweka katika utendaji kile kilichoandikwa. Wakati mwingine mchakato huu unaweza kuwa mchungu, lakini uwa na uhakika kwamba, ni kwa faida yako na itakuongoza katika ukubali wa kina wa Rafiki yako Yesu na ukweli wake. Je, ni haja yako leo kuruhusu Neno la Mungu kupanya ndani ya moyo wako, kukatilia mbali kile ambacho kinakuharibu ili aponye Maisha yako?

### **Mambo ya Kuombea**

- Omba Mungu azungumze kwako kwa uwazi katika Neno lake leo.
- Omba kwa ajili ya ushawishi na moyo ulio tayari kupokea upanga mkali wa Neno, hata kama linakata.
- Omba kwa ajili ya ufanisi na nguvu ya Roho Mtakatifu kwa ajili ya wale amba wanatafsiri Biblia na Roho ya Unabii kwenda kwenye lugha nyingine nyingi.
- Omba kwamba Mungu atusaidie kila mmoja awe mwinjilisti wa vitabu ili kwamba tuweze kushiriki machapisho ya “Glow Tracts” au neno kwa majira kwa wale waliochoka.
- Omba kwa ajili ya shule zetu na taasisi za elimu ili wawe wakweli kwa Neno la Mungu na kwa utume wake kwa vijana wadogo.

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:  
<https://247unitedprayer.org>

## Siku ya Kumi na Sita – May 18

### Neno – Liletalo Uzima

*“Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki.”* – 2 Timotheo 3:16

*Uhai wa Mungu, ambao unatoa uzima kwa ulimwengu, ni Neno lake. Ilikuwa ni kwenye Neno lake kwamba Yesu aliponya magonjwa, na kukemea mapapo. Kwa Neno lake alituliza badari na kufufua wafu; na watu wakashuhudia kwamba Neno lake lilikuwa na nguvu isiyo ya pekee. Alisema Neno la Mungu kadiri alivyolinena kwa waandishi wote wa Agano la Kale. Biblia yote ni udhihirisho wa Kristo. Ndicho chanzo pekee cha nguvu yetu.* Gospel Workers, uk. 250

### Changamoto ya Moyo.

Si ni ajabu kwamba Biblia, ambalo ni Neno la Mungu ni zaidi ya mkusanyiko wa maandiko ya kale? Imevuviwa, ikimaanisha kwamba Mungu alihusika moja kwa moja katika kusaidia waandishi waaminifu kuweka katika karatasi mawazo aliyovuvia Mungu. Katika maneno yake yaletayo uzima, na nguvu ya kurejesha iletayo badiliko katika Maisha na kurejesha, na kuponya imezamishwa ndani yake. Lakini linawekwa hai na Imani.

Je, unaamini kwa kweli kile ambacho Mungu anasema ndani ya Neno lake? Je, ni lini mara ya mwisho ulipomchukulia Mungu kwa Neno lake na kuamini kwamba kile alichoahidi atakifanya, hata kama hisia zetu zinatuambia kinyume chake? Je, utaruhusu Neno la Mungu kuhuisha na kurejesha roho yako leo.

### Mambo ya Kuombea

- Omba kwa ajili ya uwezo wa kuwa na Imani katika ahadi za Mungu na siyo kukokotwa na hisia zako za mashaka na hofu.
- Omba ahadi za Neno la Mungu kwa yale majina ya watu 7 walio katika orodha yako.
- Omba kwamba upendo wa Yesu na ukweli wa Neno lake upate upenyo kwenye nchi ambazo hakuna uwepo wa kanisa la Waadventista wa Sabato
- Ombea waumini ambao wanapitia uzoefu wa mateso ya kidini hasa katika nchi za Urusi, China na Mashariki ya Kati.
- Ombea wale waliochagua kubatizwa tangu mgogoro ulipoanza katika Ulaya Mashariki. Omba kwamba hayo maamuzi yadumu.

## Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

## Siku ya Kumi na saba – May 19

### Neno – Nuru

*“Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu.” – Zaburi 119:105*

*Yeye apekeaye mwali wa kwanza wa nuru ya mwanga iliyotumwa kwake, na kutembea katika nuru hiyo, anaelekeza matendo yake kuwa katika upatanifu na Neno la Mungu, na atapokea nuru zaidi. Yeye atembeaye katika nuru kwa namna nuru hiyo inavyokuja, bila kusubiri hadi mashaka yote yaondolewe, kila fumbo kufumbuliwa, atafuata na kumfahamu Bwana. Kwake yeye hiyo nuru itang’aa zaidi na zaidi hadi kwenye siku kamili. Mapito yake yataangazwa kadiri anavyosogea. Neno la Mungu litakuwa ni taa ya miguu yake na mwanga wa njia yake. Signs of the Times, 9/17/1902*

### Changamoto ya Moyo.

Je, unakumbuka siku ile ulipomkabidhi Yesu moyo wako na Maisha yako? Au wakati ambapo hubiri lililotolewa lilizungumza na moyo wako? Au wakati ule ambapo ulisoma kisa au mafungu fulani kwenye Biblia na kikakuguswa kwa ukweli?

Neno la Mungu lina nguvu. Muumbaji mwenye uwezo. Hata hivyo bado tunaonekana kupambana ili kuacha hilio Neno lifanye kazi katika Maisha yetu. Tunageukia kutumaini uwezo wetu wenyewe, akili, ushawishi, badala ya kutumaini ahadi zilizopo kwenye Biblia na kumtegemea mhunzi wa kimbingu wa Neno – Muumba mwenye uwezo wote aliye Mungu. Ni nani aliye tayari kuliko unavyodhani, kuweza kuleta katika ukamilifu utimilifu wa ahadi zake katika Maisha yako? Je, utamruhusu akamilishe kazi hiyo katika Maisha yako? Utatumainia Neno lake upya leo, uliamini, na kuliruhusu kufanya kile linachosema linaweza kufanya? Utaruhusu Neno lake liwe nuru halisi katika mapito yako?

## **Mambo ya Kuombea**

- Ombea wale watu 7 uliowaorodhesha kwa majina
- Mwombe Mungu akusaidie kupata utambuzi wa kina kutoka katika Neno lake kiasi kwamba unaweza kuwashirikisha wale watu saba unaowambea
- Omba na kudai ahadi maalum kutoka kwenye Biblia ili kuimarisha maombi yako.
- Omba kwamba sisi kama kanisa tupate kujifunza Neno la Mungu na kuomba kwa namna ambayo hatujawahi kuomba kabla ili kumwagiwa mvua ya masika.
- Ombea Myanmar kadiri mgogoro kati ya Junta unavyoendelea. Omba kwa ajili ya wigo wa ulinzi kuwazunguka waumini na kwamba waweze kubakia imara katika Imani kati ya vurugu zote hizo.

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kuitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:  
<https://247unitedprayer.org>

## **Siku ya Kumi na Nane – May 20 Ushuhuda wa Israel Ramos**

### **“Agizo la Kuhubiri Neno”**

Na Israel Ramos

Nilikuwa mwanafunzi wa sekondari lakini mwinjilisti wa viabu kule Maine. Kwa kawaida siku za Ijumaa tulikuwa huru kwani iliitwa siku binafsi, lakini program pacha iliyokuwa na wanafunzi wakubwa ilihusu uuzaaji wa vitabu vyta gharama nayo ilikuwa na baadhi ya watu waliofanya kazi Ijuma ili kupata fedha za ziada. Katika hali ile ya kufurahia fursa ya kuwa kati ya kundi lililopendwa, niliamua kubaki nao. Niliandamana nao nyumba kwa nyumba nikijaribu kuwathibitishia kwamba nilistahili kuwa kati yao wakati wenzangu walikuwa wakienda milango mingine. Baada ya muda wa saa kadhaa katika eneo la kazi, tukageuza kurudi nyumbani. Ndipo niliposikia hubiri la kizamani ambalo lingebadilisha Maisha yangu yaliyosalia.

Hayati C. D. Brooks alikuwa akizungumza kwenye radio huku spika zote za gari zikiwa zinaongea kwa sauti ya juu. Tukio lilioandamana na hubiri hilo lilikuwa ni kuwekwa wakfu kwa wachungaji wawili ili wafanye kazi ya injili. Mfano wa kuvutia uliokuwa kwenye ujumbe ulitoka katika 2 Timotheo 4:1-4, haya ni maneno ya Paulo wa zamani kwa kijana Timotheo: “Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu,

atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake; lihubiri neno."

Nilikuwa nimekamilisha masomo ya kidato cha sita, na tayari nilihisi kwamba Mungu ananiita kuwa mtumishi. Nikiwa bado katika mchakato wa kujitambua kwamba mimi hasa ni nani, haiba yangu ikihama na kuyumba kutoka katika kuwa mkimya hadi kuwa mtupu kimawazo, kuhisi ukosefu wa usalama hadi kujiatini. Hadi wakati huo, nilikuwa siyo mtu wa kukaa nisikilize hubiri kwenye radio. Kwa kweli ni hivi karibuni tu ndipo nilipokuwa Mkristo nikiacha nyuma yangu maisha ya chaguzi zilizodumaza fikira zangu na kuharibu uzoefu wangu wa kiroho. Lakini kadiri sauti ya yule mhubiri ilivyoendelea kuunguruma ikichambua mafungu, mawazo yangu – pamoja na madirisha ndani ya gari – yalioneckana kama yalikuwa tayari kulipuka. Agizo lilikuwa ni hili "Hubiri Neno!" likifuatiwa na maonyo makali dhidi ya wachungaji wanaofanya kinyume.

Mambo mawili yalitokea kuanzia siku ile na kuendelea. Kwanza nilipata shauku ya Neno la Mungu kuliko nilivyowahi kupata. Jambo la pili nilijitoa kikamilifu kutangaza ujumbe huo.

Majira ya kiangazi yalipokoma, nilirudi chuoni kwa ajili ya mwaka wangu wa kwanza. Katika mahitaji ya darasa letu kuhusu hotuba, niliamua kutumia hotuba niliyoisikia ndani ya gari kama msukumo wangu. Nikiwa sijali kuchukua kazi za wengine na kutumia wakati huo, nilijaribu kadiri nilivyoweza kukumbuka lile hubiri nililosikia miezi michache iliyopita. Jambo pekee nilokumbuka wazi wazi lilikuwa hubiri la Paulo akimwagiza Timotheo kuwa, "Hubiri Neno!"

Kusema kweli kabisa, wasilisho halikuleta maana yoyote. Nilishindwa kutambua kwamba hakuna yejote katika hadhira ile aliyekuwa akikusudia kuchukua fani ya uchungaji. Hata hivyo tulikuwa ni kikundi cha vijana waliomaliza kidato cha sita tukijaribu kutimiza matakwa ya kazi tuliyopewa ili kumaliza kozi kwa ukamilifu, ambayo hata hivyo haikuwa ya kuvutia sana kwa sababu ya hitaji hilo la kusimama na kuzungumza hadharani. Pamoja na kutokujua mahitaji ya hadhira yangu, mimi pia sikuwa nimefikiria uwezo wangu kama mzungumzaji. Nikiwa na msukumo wa mtindo wa hayati Brook, nilikuwa nimeandika hubiri likiwa limejawa na alama za mshangao, nikijiona mwenyewe nikiongea kwa sauti yangu yote kwa wenzangu kana kwamba mimi pia nilikuwa nikiwatia moyo katika kuwekwa kwao wakfu. Wasilisho langu halikurandana kabisa na kusudi langu.

Hata sikumbuki alama nilizopata darasani kwa hotuba hiyo. Ninakumbuka tu vipande vya ushauri kutoka kwa mkuu wa chuo akinikumbusha kuwa nisibabaishe na Biblia

yangu, ikifuatiwa na maneno ya kutia moyo kwamba, "Mungu atakutumia siku moja kumfanya kitu fulani maalum."

Maneno hayo yalihitaji Imani. Mimi nilikuwa ni mwanafunzi niliyekuwa nikihangaika katika kila somo, na shauku kubwa moyoni kutoa Maisha yangu katika kumtumikia Mungu ilikuwa haijajitokeza katika Maisha yaliyojitoa kikamilifu. Kadiri nilivyojaribu sikuweza kuelewa Biblia mimi mwenyewe. Kwa mwaka mzima, aya pekee niliyoweza kujifunza kwa ajili ya wakati wangu wa kesha asubuhi ilikuwa ni 2 Timotheo 4:1-4

Takribani miaka kumi na mitabo baadaye, aya hizo hizo zilisomwa kwangu katika huduma ya kuniweka wakfu. Sasa imekuwa ni miaka ishirini na tano tangu siku ile nilipojihubiria mwenyewe. Na hayo maneno ya Paulo yenye msukumo bado yanatumika kutia moyo na kutoa maonyo ili kutimiza huduma yangu.

*Israel Ramos ni mkurugenzi na mratibu wa huduma ya kitivo cha umma katika Konferensi ya Lake Union, na Michigan. Mke wake aitwaye Judy ni mkufunzi na wote pamoja wana Watoto watatu wa kiume ambao wanashiriki nao Maisha kwa furaha.*

### **Changamoto ya Moyo.**

Ikiwa wewe ni mchungaji au siyo, kila muumini ameitwa kushiriki huu ujumbe wa Biblia unaobadilisha Maisha. Kwa namna yoyote ile tunayoshiriki Imani yetu na wengine, katika kuhubiri, kufundisha, kuandika, kuimba, katika vitendo vya huduma, au njia nyingine zozote za ubunifu, ni muhimu kwamba, kile tunachoshiriki kiwe kimejawa na Neno la Mungu na kiwe kinatolewa kwa uaminifu. Katika kuoanisha mwelekeo wake na tabia ya Mungu ya upendo.

Neno la Mungu lina nguvu. Zoezi la kulihubiri linagusa Maisha kwa umilele. Je, utajibu wito wa Paulo wa "Kuhubiri Neno" kupitia kwa maneno yako na matendo yako?

### **Mambo ya Kuombea**

- Omba kwa ajili ya ujasiri wa kuhubiri Neno kwa maneno na kwa vitendo leo. Omba kwamba vijana wengi waitwe ili kuhubiri Neno.
- Omba kuhusu swalii lolote ulilo nalo katika Biblia. Mwombe Mungu akusaidie kupata majibu na ufasaha kuhusu maswali haya.
- Waombee wachungaji wa eneo mahalia. Omba kwamba Mungu awategemeze, awalinde na muhimu zaidi, awajaze na Roho Mtakatifu kwa wingi
- Omba kwa ajili ya ulinzi wa vijana kutoka kwenye uraibu wa teknolojia na muda mwangi kwenye viambaza vya simu unaoongezeka siku baada ya siku

- Waombee wale watu 7 waliopo katika orodha kwa kuwataja majina yao mmoja mmoja. Endelea kudai ahadi za Mungu.

## Siku ya Kumi na tisa – May 21

### Sabato ya Mambo ya Kuombea

- Omba kwa ajili ya mkutano mkuu unaokuja katika Konferensi Kuu kule St Louis, Marekani tarehe 6 hadi 11, 2022
- Omba kwamba tuwe na “Uzoefu wa Chumba cha Juu” kama wanafunzi wa Yesu walivyokuwa nao wakati wa Pentekosti, na kwamba tuwezeshwe kufikia ulimwengu wote kwa ajili ya Yesu kama wao walivyoweza.
- Omba kwamba ule wakati maalum wa maombi katika mikutano uwe na maana yenye kina na kuwa wa msaada kwa wote watakaohudhuria.
- Omba kwa ajili ya umoja katika mikutano yote ukijengenka katika kuheshimu Neno la Mungu, maombi ya unyenyekevu, na uwezo wa Roho Mtakatifu.
- Omba kwa ajili ya kujihusisha kikamilifu katika utume wa kanisa linapotangaza ujumbe wa Malaika watatu wa Ufunuo 14 na yule wa nne wa Ufunuo 18k.

## Siku ya Ishirini – May 22

### Jumapili ya Mambo ya Kuombea

- Omba kwamba Mungu azungumze ndani yako kupitia katika Neno lake leo.
- Omba kwamba Mungu akusaidie kudumu bila kukatisha ibada ya kesha kila siku juma linalokuja.
- Omba kwamba Mungu aamshe upya shauku katika miyo ya watu wake – shauku mpya kwa Neno lake, kwa maombi, na kwa utume
- Omba kwamba isiwe ni biashara kama kawaida katika mikutano mkuu wa Konferensi Kuu, lakini uamsho wa kiroho ambao utatuwezesha kuufikia ulimwengu huu kwa ajili ya Yesu.
- Ombea vijana na watu wazima watakaohudhuria mikutano mkuu katika Konferensi Kuu, ili kwamba wamwone Yesu akidhihirishwa na kwamba wawe na ari ya kumfuata na kumfahamu zaidi.

Vyanzo vingine vya kukusaidia kuzama kwa kina.

[Evangelism - Preaching Sermons and Resources](#)

**Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

**Juma la 4: Mei 23 – 29**

**Siku ya Ishirini na Moja – May 23 – Wazo la Kesha: Kristo Haki Yetu**

## **“Ondoka Uangaze”**

Na Frank Fournier

Hivi karibuni, “dunia itaangazwa” kwa vigezo vya utukufu wa tabia ya Mungu. Wengi wenye dhambi waliokombolewa wataodoka na kuangaza kwa uwezo wa Mungu wakivuta majeshi ya wamataifa katika mikono ya Baba aliye tayari kuwapokea. Ufunuo 18:1, Isaya 60:1-5

Tumeambiwa kwamba siku zinazokuja, mvuto wa Roho Mtakatifu utakuwa na nguvu kiasi kwamba ulimwengu utaghubikwa na hali ya ajabu ya kushawishika. Wakristo wasio na ubinafsi wataonekana wakikimbia kutoka kwa mtu huyu kwenda kwa mwingine, kutoka nyumba moja kwenda nyumba nyingine wakizungumza maneno waliyopewa moja kwa moja kutoka mbinguni.

Maelfu, au pengine mamilioni wataitikia. Midomo yao itavuma kwa wimbo mpya, kwani kwa majeshi yote ya Mungu hawamwoni ye yote ila Yesu pekee.

Katika mjadala wa Shule ya Sabato siku chache zilizopita, mmoja wa washiriki wetu alidokeza kwamba mwanadamu mwenye mwili anatamani kuwa mtu fulani. Anatamani angetambuliwa kwa sababu ya kitu fulani. Lakini matumaini kama hayo ni matumaini potovu. Yesu alisema kuwa, “Pasipo mimi, ninyi hamwezi kufanya neno lolote.” Kwa hiyo chochote tunachotekeleza, ni kwa uwezo wa Mungu ndani yetu. Kule kujisifu kwa kile ambacho Mungu pekee ndiye awezaye kukifanya ni kumfedhehesha na ni hatari sana kwetu kiroho. Yesu pekee ndiye aliye wokovu wetu, yeye peke yake ndiye utukufu wetu, haki yetu na yote katika yote.

Kwa muda mrefu Mungu amejizuia kujidhihirisha mwenyewe, upendo wake, hekima yake na nguvu zake kwa ulimwengu unaoangamia, ila tu kama watu wake wangemwezesha kupitia katika mwenendo ambao angeutumia badala ya hali ya kujitosheleza inayoonekana, “...tumempa mpaka Mtakatifu wa Israeli.” (Zaburi 78:41).

Tunagusana na uhalsia ambao hatuwezi kujisikia hivyo kwa kujiona "Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu;" (Ufunuo 3:17)

Nabii akasema, "Nikaona kwamba nguvu za Watoto wa Mungu ziko kwenye unyenyekevu wao. Wanapojiona wadogo katika macho yao wenyewe, Yesu atakuwa nguvu zao kwao na haki yao, na Mungu atafanikisha kazi yao." 3T 307.1

Mungu anasema kuwa, "...lakini mtu huyu ndiye nitakayemwangalia, mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo neno langu." (Isaya 66.2)

"Maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye jina lake ni Mtakatifu; asema hivi; Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu; tena pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekua, ili kuzifufua roho za wanyenyeku, na kuifufua miyo yao waliotubu." (Isaya 57:15)

Kulingana na Ellen G. White, "Wakala wa kibinadamu anayefanya kazi kwa ufanisi anakuwa na hisia kubwa kuhusu udhaifu na kutokustahili kwake, na anamkabidhi Kristo roho yake isiyokuwa na msaada. Hii ndiyo tabia ambayo Mungu anaiita 'yenye majuto.' Hapa ndipo penye chimbuko la nguvu zetu." 1888 Material 1468.1

Je, ni lazima tungoje hadi 'kila msaada wa kidunia umeondolewa? DA 121. Tunahitaji kushushwa na kudhalilishwa hadi tujione bure kabla hatujahisi hitaji letu la mkono wa Mungu wenyе msaada? Je, tunasubiri mateso ya mwisho ili kunyenyekiza miyo yetu? Tunahitaji kusikia maneno haya: 'Tazama bibi-arusi anakuja' kabla hatujainuka kwa sababu ya tukio?

Yesu anakuja hivi karibuni. Amkeni watu wa Mungu!

Zoezi la kumheshimu Mungu mbele ya ulimwengu halitakuwa rahisi. Miyo yetu haitabadili na kuitikia haki ya Kristo kuliko ilivyo sasa hivi. ni lazima tunyenyekiza miyo yetu sasa tukijenga katika uhitaji wetu na kushikilia nguvu za Mungu wakati huo huo tukijenga katika ahadi zake.

Amri ya Mungu kwetu leo ni hii:

"Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, Na utukufu wa Bwana umekuzukia. Maana, tazama, giza litaifunika dunia, Na giza kuu litazifunika kabilia za watu; Bali Bwana atakuzukia wewe, Na utukufu wake utaonekana juu yako. Na mataifa watajilia nuru yako, Na wafalme kuujia mwanga wa kuzuka kwako. Inua macho yako, utazame pande zote; Wote wanakusanyana; wanakujia

wewe; Wana wako watakuja kutoka mbali. Na binti zako watabebwa nyongani. Ndipo utakapoona na kutiwa nuru, Na moyo wako utatetemeka na kukunjuka; Kwa kuwa wingi wa bahari utageuzwa kukujia, Utajiri wa mataifa utakuwasilia.” (Isaya 60:1-5)

*Frank Fournier ni mchungaji wa Eden Valley Church katika taasisi ya Eden Valley kule Loveland, Colorado.*

### **Changamoto ya Moyo.**

Unyenyekevu ndiyo ufunguo wa mafanikio katika Maisha ya Mkristo, kwani kadiri tunavyotambua uhitaji wetu ulio mkuu, tunajikabidhi kwa Yeye yule ambaye ana haki yote tunayohitaji, naye atatupatia ushindi. Je, hauhitaji ushindi dhidi ya dhambi ya ubinafsi, na nguvu katika kuongoa roho? Hautamani kupokea kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kila siku? Kwa kweli hauhitaji Yesu akae ndani yako na kupidia kwako, akidhihirisha tabia yake ya upendo, kujitoa kafara na neema kwa wote unaokutana nao? Ni nini leo kinakuzuia kuishi katika haki ya Kristo? Je, kuna haki binafsi katika Maisha yako? Ni hofu gani unazoweza kuwa unashikilia unapajaribu kushiriki upendo na ukweli wako kwa ujasiri na watu walioko katika eneo lako la mvuto?

Jipe moyo, Yesu atakusaidia kama utamwendea katika uhitaji wako. Anasema kuwa, “Wote anipao Baba watakuja kwangu; wala ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe.” (Yohana 6:37). Yuko tayari kuangaza utukufu wake kupidia katika Maisha yako kuanzia leo. Kwa nini usimwombe ajitukuze katika Maisha yako sasa hivi?

### **Mambo ya Kuombea**

- Omba kwa ajili ya uelewa dhahiri wa “Haki kwa Imani” kati ya waumini.
- Omba kwa ajili ya moyo ulionyenyekea na kipawa cha kujisalimisha.
- Omba kwa ajili ya ujasiri wa kushiriki Neno la Mungu na watu wanaokuzunguka kupidia katika kushiriki masomo ya Biblia ukifundisha na kuhubiri.
- Omba kwa ajili ya ujasiri katika kushiriki upendo na ukweli wa Mungu kupidia katika karama zako za pekee.
- Omba kwamba kadiri tunavyotambua ukaribu wa kurudi mara ya pili kwa Yesu, wote tutumie muda kumtafuta kwa miyo yetu yote na kuchimba ndani zaidi katika Neno lake.

### **Vyanzo vingine vya kukusaidia kuzama kwa kina.**

[Righteousness of Christ Made Simple – From Pigpen to Salvation – Series by Frank Fournier](#)

**Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

## Siku ya Ishirini na Mbili – May 24

### Sayansi ya Sayansi Zote

*“Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu viliyuo juu ya nchi, au viliyuo mbinguni.”* – Wakolosai 1:19-20

*“Sayanasi ya ukombozi ndiyo sayansi ya sayansi zote, sayasni ambayo ni somo wanalojifunza Malaika na viumbe wote wa malimwengu ambayo hayakuanguka, sayansi inayohusisha usikivu wa Bwana na Mwokozi: sayansi ambayo itaingia katika kusudi lililoko katika akili za Yule asiye na mwisho – ikihifadhiwa kwa ukimya nyakati zote hata milele. (Varumi 16:25): sayansi itakayokuwa somo kwa waliokombolewa wa Mungu katika vizazi visivyokoma. Hili ndilo somo la juu analoweza kujihusisha nalo mwanadamu: Kuliko somo jingine lolote analoweza, litakalosisimua akili zake na kuinua roho yake.* Education, uk. 126

### Changamoto ya Moyo.

Je, una digrii? Unaenda shuleni? Umejifunza stadi? Mambo haya yote ni mema, lakini hakuna kinachoweza kulinganishwa na somo la sayansi ya wokovu. Ni rahisi tu kusema, Naam, ninafahamu Yohana 3:16 na kudai kwamba unaelewa ukombozi. Na wakati wokovu unaweza kuelezwaa kwa namna iliyo rahisi, bado kuna undani wa somo hilo, ambao unahitaji kuangaliwa kwa kina. Kuzama katika somo hili, kufikiria kupitia katika mambo ambayo Yesu alikamilisha kupitia katika Maisha, kifo, na ufuluo wake, na kutambua jinsi yanavyohusiana na dhana ya pambano kuu, hekalu, hukumu na muhimu zaidi, kwa Maisha yetu ya kila siku; yote haya yatakusaidia kuzama katika upendo na Yesu kwa kuongezeka zaidi na zaidi kadiri unavyoingia ndani zaidi.

Je, leo hii utachagua kujihusisha na sayasi hii ya sayansi zote? Utatenga muda kwa ajili ya somo hili muhimu la milele, jinsi ya kuongoa roho kwa ajili ya ufalme wa Mungu?

### Mambo ya Kuombea

- Omba kwamba upate uelewa wa kina wa kazi ya wokovu ambayo Yesu alikamilisha kwa ajili yako.

- Ombo kwa ajili ya uelewa dhahiri wa kile kilichotokea pale msalabani.
- Ombo kwa ajili ya wingi wa watu ambao hawaelewii ukweli wa ajabu wa Kristo aliye haki yetu na injili ya wokovu ambayo inatoka kwake kwa ujumla wake, wala siyo kazi za mwanadamu.
- Ombo kwa ajili ya jamaa zako wa karibu. Ombo kwa ajili ya wokovu wao na kwa ajili ya fursa za kushiriki nao Imani yako, Neno la Mungu na upendo wa Kristo.
- Ombea wale wanaopambana na uraibu wapate kushinda.
- Ombea majina ya wale watu 7 katika orodha yako. Ombo kwa ajili ya fursa ya kuwasiliana nao na kuwaalika kanisani au nyumbani kwako kwa ajili ya mkutano.

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

### **Siku ya Ishirini na Tatu – May 25**

#### **Haki ni nini?**

*“Heri wenye njaa na kiu ya haki; Maana hao watashibishwa.” – Mathayo 5:6*

*Haki ni utakatifu, kufanana na Mungu, na ‘Mungu ni upendo.’ 1 Yohana 4:16. Ni ulinganifu kwa sheria ya Mungu, maana ‘maagizo yako yote ni haki’ (Zaburi 119:172), na ‘upendo ndio utimilifu wa sheria’ (Warumi 13:10). Haki ni upendo, na upendo ni nuru na uzima wa Mungu. Haki ya Mungu imejumuishwa ndani ya Kristo. Tunapokea haki kwa kumpokea yeye. – Thoughts from the Mount of Blessings, Uk. 18.*

#### **Changamoto ya Moyo**

Je, una njaa na kiu ya haki ya Kristo?

Maisha yake ya upendo kamili usio na ubinafsi na kifo chake cha mbadala hukupatia zawadi iliyo na pande mbili za neema yenye kutetea: 1) Haki yake iliyoambukizwa, ambayo ni ahadi kwamba umefunikwa kwa maisha yake makamilifu kupitia kwa Imani katika ahadi hiyo. 2) Haki yake iliyogawiwa, ambayo ni ahadi kwamba atakubadilisha kutoka katika kuwa mbinafsi, hata uwe kiumbe ambaye huangaza upendo usio na ubinafsi wa Yesu, kupitia Imani iliyo hai katika ahadi hiyo.

Zawadi hii yenyе pande mbili itakukamilisha; itakuridhisha kweli kweli; itakuokoa! Zawadi hii inatolewa kwako kupitia kwa Yesu. Bure. Kwa nini usiikubali leo na kuanza kuishi maisha yenyе furaha na yaliyojawa na Yesu katika utambuzi wa uhalisia huu mzuri wa upendo wa Mungu wenye kukomboa?

### **Mambo ya Kuombea**

- Omba ili Mungu akusaidie kuacha kuamini udanganyifu wa Shetani unayokufanya ufikiri kwamba haustahili upendo wake.
- Omba na kumsihi Mungu kuambukiza na kugawa haki yake kwako.
- Omba kwamba wafanya kazi wasio Wakristo wanaofanya kazi wakati wa mikutano ya Halmashauri Kuu ya Kanisa wahisi upendo wa Mungu na uwepo wake ndani ya wajumbe na kuwaongoza kutaka kufahamu zaidi kuhusu Waadventista wa Sabato.
- Omba kwa ajili ya masuala yote ya utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa watu katika mkutano wa Halmashauri Kuu ili yaende vizuri kama yalivyopangwa.
- Omba kwa ajili ya wale walio katika dirisha la 10/40 ambao hawajawahi kusikia ukweli huu mzuri na wana dhana iliyoharibiwa ya upendo na tabia ya Mungu.

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

### **Siku ya Ishirini na Nne – May 26**

### **Mvuto wa Yesu Usiofananishwa**

*“Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo; tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani.” – Wafilipi 3:8-9*

*Kadiri mwanafunzi wa Biblia anavyomtazama Mkombozi, ndani ya roho kunakuwa na kuamshwa kwa nguvu ya ajabu ya Imani, kuabudu, na upendo. Macho huelekezwa katika njozi ya Kristo, na mtazamaji hukua na kufanana na kile anachokipenda. – Education, 192.*

*Unapaswa kuichunguza Biblia; kwani hukueleza kuhusu Yesu. Kadiri unavyosoma Biblia, utaona mvuto wa Yesu usiokuwa na mfano. Utampenda Mwanamume wa Kalvari. – LS, 293*

### **Changamoto ya Moyo**

Je, moyo wako unatamani kuelewa “mvuto wa Yesu usiokuwa na mfano” – kumfahamu na kumpenda Yesu kuliko vingine vyote? Je, unajiuliza jinsi ya kuwa na uhusiano kama huo pamoja naye? Kuwa na ujasiri! Elekeza macho yako kwake. Jifunze kwa maombi matukio ya maisha na kifo chake. Tambua zawadi ya pekee ya kafara yake na uhalisia kwamba alifanya haya kwa ajili yako, wewe binafsi. Tafakari ukweli kwamba anakupenda, na anakuthamini zaidi hata ya maisha yake ya milele. Amini kwamba msamaha wake ulitolewa kwa ajili *yako*, na haki yake inatosha. Tafakari mambo haya, na ruhusu mvuto wa Yesu usiofananishwa uweze kuyeyusha moyo wako leo.

### **Mambo ya Kuombea**

- Omnia kadiri unavyojifunza Neno la Mungu ili Roho wake aweze kudhihirisha ndani ya moyo wako mvuto wa Yesu usiofananishwa na kukuingiza ndani zaidi katika furaha ya kumfahamu Yesu binafsi.
- Omnia kwamba Mungu adhihirishe miungu yoyote katika maisha yako ambayo inaweza kukuvuruga usiouone uzuri wa Yesu kwa uwazi.
- Omnia ili Mungu akusaidie kushiriki upendo wake kwa wale wanaokuzunguka kwa namna halisi na mahususi.
- Omnia kwamba Mungu alete viongozi wacha Mungu, wanaofundishika na wanyenyekevu kwa ajili ya siku za usoni; viongozi watakaotoa uongozi uliojikita kwa Kristo kadiri kanisa lake litakavyokuwa likikamilisha mamlaka yake ya kimbingu katika ulimwengu.
- Omnia kwamba wajumbe wa mkutano wa Halmashauri Kuu waombe kwa dhati ili mapenzi ya Mungu yaweze kutimizwa, na kisha kujisalimisha katika mapenzi yake, vyovyo itakavyokuwa.

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:  
<https://247unitedprayer.org>

## Siku ya Ishirini na Tano – May 26 Ushuhuda wa Andy Im

### **“Yeye Aliyeanzisha kazi njema ndani yako ...”**

Na Andy Im

Nilipoamua kutoa maisha yangu kwa Kristo kwa mara ya kwanza wakati nikisoma chuo, uzoefu wangu kwa hakika haukuwa kile nilichokitarajia. Badala ya furaha na Amani ambayo wengine waliizungumzia, maisha yangu ya siku kwa siku yalijawa na wasiwasi na hisia za hatia nzito.

Nilihisi kama sikuwa mwema sana, na mara kwa mara nilikuwa nikibonyeza kitufe cha “rekebisha” baada ya kila kushindwa kunakoonekana. Nilijaribu sana kuwa mkamilifu katika kile nilichokula, mazoezi, maisha ya maombi, na tabia za kila siku.

Lakini kamwe sikuwahi kufikia yale niliyofikiria kuwa ni vipengele muhimu vya kuwa Mkristo Mwadventista Msabato halisi. Hatimaye nilifikia hitimisho kwamba naamua kudumu na Ukristo lakini nichanganyikiwe kutokana na hatia, au niache yote hayo nyuma kwa pamoja ili kufurahia starehe za dunia.

Nilichagua hilo jambo la pili, na nikajambia, “Ikiwa nitafurahia dunia na kupotea, ninaweza pia kuifurahia vizuri.”

Nilihamu kutoka katika jambo moja kwenda lingine na kujiingiza kikamilifu katika vishawishi vya dunia. Nilipitia uzoefu usio wa asili wa kichochezi cha kujihisi kuwa “juu” kwa namna nyingi sana. Lakini, haukupita muda mrefu kabla sijatambua kwamba dunia ilikuwa ni mtaa ulio na mwisho na nikajikuta kwa mara nyingine katika shimo la kukata tamaa.

Usiku mmoja, nilianza kupata hisia za wasiwasi zisizo za kawaida baada ya kujidunga kitu fulani. Uzoefu huo ulikuwa wenye karaha na kutisha, lakini hapakuwa na namna yoyote ya kuepuka hatari niliyojikuta ndani yake.

Nilikuwa nimekata tamaa.

Ndipo wakati huo niliangaza chumbani kwangu na kuona Biblia ambayo mama yangu alikuwa ameniachia. Niliichukua na kufungua kitabu cha Zaburi na kuanza kusoma.

Nyakati chache baadaye, nilianza kuptitie kitu cha ajabu sana. Nilipokuwa nikisoma Zaburi, wasiwasi ulianza kupotea na nilijikuta katika hali ya kutambua kile nilichokuwa nikisoma na kukiingiza kichwani.

“Kuna nguvu katika neno,” niliwaza mwenyewe. Jinsi wasiwasi wa madawa ya kulevyia unavyoweza kuondoka kwa kusoma Maandiko ulikuwa unakaribia kuwa muujiza ambao sijawahi kuupitia.

Kilichonishangaza sana usiku ule nilipokuwa nikisoma Zaburi ilikuwa ni taswira iliyowasilishwa ya Mungu kama Mtu aliyekuwa kwa ajili yangu – alikuwa upande wangu! Mungu hakuwa mwenye kulipiza kisasi, akitafuta kunisulubisha kwa makosa. Niliona mfano wa Mtu anayehurumia watoto wake kwa namna ile ile ambavyo baba huwahurumia watoto wake (Zaburi 103:13). Niligundua kwamba Mungu hakuwa tayari kunikamata, na kwamba hakukuwa na hali au hatari ambayo Mungu asingeweza kuniokoa nayo (Zaburi 139:1-10).

Usiku ule ulikuwa wa kwanza baada ya siku nyingi, ambapo nilitumia muda kugundua na kusoma kuhusu vile Mungu alivyo hasa. Na hilo hufanya tofauti yote duniani. Jinsi mtu anavyohusiana na kumtambua Mungu hutambulika zaidi kwa vile tunavyomfahamu kuwa ndivyo alivyo.

Lakini hilo si jambo pekee linalogusa uzoefu wa mtu kama Mkristo. Pia niligundua mafundisho ya pekee ya wokovu upatikanao kupitia kwa Imani ya mtu kwa kazi YAKE ili kukamilisha kile ambacho hatuwezi kufanya sisi wenyewe, licha ya hali za sasa au za siku za usoni, bila kujali zilivyo za kuhuzunisha.

Biblia inatuarifu kwamba mchakato wa wokovu ni kazi ya Mungu ndani yetu. Ni jukumu lake kufanya yasiyowezekana, yawezekane ili mradi tu tumpatie ruhusa ya kufanya kazi ndani yetu ili aweze kutenda yanayompendeza (Wafilipi 2:12, 13).

Uzoefu wa wokovu pia ni mchakato unaochukua muda kunyoosha mikunjo, hitilafu ambazo nyakati fulani tunazihisi katikati ya kile tunachokifahamu kuwa ndicho sahihi dhidi ya hatari na uzoefu wetu wa sasa.

Popote pale ulipo katika uzoefu wako, bila kujali matarajio yalivyo ya kuhuzunisha, ni muhimu kufahamu kwa Imani – na siyo kwa hisia zako – kwamba Mungu anakusaidia. Kwamba atakamilisha kazi ambayo kwa hakika, Yeye mwenyewe alianzisha.

Katika maneno ya Maandiko tunaweza kuamini jambo hili, “ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema miyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu” (Wafilipi 1:6).

Yesu anakualika leo kuweka kabisa wokovu wako mikononi mwake. Upo katika mikono salama unapofanya hivyo. Niamini.

*Andy Im anahudumu kama mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhuru wa Dini katika Konferensi ya Michigan na anafurahia kupiga picha, kuvua samaki, na kucheza mchezo wa piko katika muda wake wa ziada. Amefunga ndoa na Laura, na wana watoto wakike wawili – Olivia na Karis.*

### **Changamoto ya Moyo**

Je, si jambo la kutia moyo kufahamu kwamba Mungu yupo tayari kukusaidia? Kwamba yupo kwa ajili yako, na si dhidi yako? Kwamba amejitoa si tu kuanzisha kazi njema,

lakini pia kuimaliza? Anachohitaji kutoka kwetu ni idhini yetu na utii wa kujisalimisha, kadiri anavyofanya ukombozi ndani yetu.

Je, utampatia ruhusa kamili ya kuingia moyoni mwako na katika maisha yako leo? Je, utamruhusu si tu kuwa Mwokozi wako, lakini Bwana wako, akitawala kikamilifu kila eneo la maisha yako? Je, utaamini haki yake, na kwamba anafahamu vema zaidi jinsi ya kuimaliza kazi njema aliyoianza ndani yako?

### **Mambo ya Kuombea**

- Omba kwamba Mungu aweze kunyamazisha madanganyo ya adui na kukuonyesha kwamba yupo kwa ajili yako na siyo dhidi yako.
- Omba uweze kuamini haki yake ya kukuokoa, na kwamba kujihesabia haki kwa aina yoyote kupate kuondolewa.
- Omba kwa ajili ya ongezeko la msisitizo wa kuwafikia watu kwa vikundi vidogo katika kanisa lako mahalia ili washiriki wote waweze kushiriki katika ushuhudiaji binafsi.
- Omba kwamba uweze kuwa na nguvu ya kufuata kanuni za Mungu za afya, si kama kiwango kigumu, lakini kuwezesha akili na moyo wako kuwa na ulinganifu na Roho Mtakatifu.
- Omba kwa ajili ya majina yako 7. Omba kwa ajili ya jinsi ya kupiga hatua za kuweza kuwafikia.

### **Siku ya Ishirini na Sita – May 28**

#### **Sabato ya Mambo ya Kuombea**

- Omba kwa ajili ya Mkutano ujao wa Halmashauri ya Kanisa huko St. Louis, Marekani (Juni 6-11, 2022).
- Omba kwa ajili ya familia na mahusiano yaliyovunjika katika maisha yako.
- Muombe Munguakuonyeshe mtu ndani ya kanisa lako katika juma hili unayeweza kujenga urafiki naye, ambaye hujawahi kumfikia hapo awali.
- Omba kwa ajili ya washiriki wa kanisa katika eneo lote la Mashariki ya kati, hasa huko Iran na Israeli.
- Omba kwa ajili ya wale walio katika magereza ya kimwili na ya kiroho. Omba kwamba kweli za Neno la Mungu ziweze kuwaweka huru.

## Siku ya Ishirini na Saba – May 28

### Jumapili ya Mambo ya Kuombea

- Omba kwa ajili ya viongozi wa kiserikali katika mji, mkoa, na taifa lako, ikiwezekana wataje kwa majina.
- Omba kwa ajili ya asilimia 30 ya washiriki wa kanisa (hii asilimia ni takribani Waadventista 13,000 wa Ukraini) ambao wanapoteza makazi yao au wanalazimishwa kuyaacha.
- Omba kwa ajili ya washiriki wa kanisa katika nchi nyingine ambao wamefungua nyumba zao kwa ajili ya wakimbizi.
- Omba ili nia ya Mungu iweze kukamilishwa ndani ya maisha yako leo. Omba kwa ajili ya miadi ya kimbingu.
- Omba Neno la Mungu kwa ajili ya majina yako 7. Wafikie na kuwafahamisha kwamba unawaombea. Waulize kile unachoweza kuombea katika maisha yao.

Vyanzo vingine vya kukusaidia kuzama kwa kina.

Praying the Word: Prayer and Promises

**Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:  
<https://247unitedprayer.org>

**Juma la 5: Mei 30 – Juni 5**

**Siku ya Ishirini na Nane – May 30 – Wazo la Kesha: Roho Mtakatifu**

**“Umwagwaji wa Roho Mtakatifu”**

Na Ron Clouzet

Katika siku ya Pentekoste ya mwaka 31 BK, Roho Mtakatifu alimwagwa kwa kiwango kikubwa katika Kanisa jipya la Agano Jipy. Matokeo yalikuwaje? Wanafunzi wa Yesu 120 waliokuwa wakiomba katika Chumba cha Juu walijazwa Roho Mtakatifu (Matendo 2:1, 4), watu ambao waliwahi kukwepa kushuhudia kwa ajili ya Yesu (Mathayo 26:69-75) walikuwa jasiri kwa ajili ya Yake (Matendo 2:14-21; 4:7-13), na wasafiri wa Kiyahudu 3,000 kuelekea Yerusalemu wakawa ndilo kundi la kwanza la Wakristo katika historia – wote katika siku moja (Matendo 2:38-41).

Kisa hiki kinapatikana katika Matendo 2, lakini sura ya 2 ya Matendo kamwe isingeweza kutokea bila sura ya 1 ya Matendo. Tunapaswa kutambua mambo mawili kutoka katika Matendo 1. Wanafunzi waliungana, wakiomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu (Matendo 1:13-14), na walikuwa wakipitia upya huduma ya Yesu ya kujitoa kwa niaba yao (tazama kitabu cha Ellen White cha *The Acts of Apostles*, uk. 35-38). Illichukua siku 10 tu kuona kile walichoshindwa kuona hapo kabla: upendo wa Mungu wa ajabu.

Hivi ndivyo vigezo viwili ambavyo bila hivyo kanisa haliwezi kutegemea kumwagwa kwa Roho wa Mungu kwa nguvu kubwa ili kumaliza kazi duniani: Kalvari na Jumuiya. Hivi ni vigezo vya msingi vya kumwagwa kwa upendo wa Mungu ndani ya mioyo yetu (Warumi 5:5).

Kanisa linapoamua kujikita katika upendo na huduma ya Yesu kwa niaba yao (Kalvari) na wanaposihi pamoja katika kutafuta kumwagwa kwa Roho Mtakatifu (Jumuiya) kanisa hilo litapata nguvu kubwa ya Mungu kwa niaba yao.

“Baada ya kushuka kwa Roho Mtakatifu, wanafunzi walijazwa sana na upendo kwake, na kwa wale aliowafia, mioyo ile iliyeyushwa kwa maneno waliyozungumza na maombo waliyotoa. Walizungumza kwa nguvu ya Roho; na kwa ushawishi wa nguvu hiyo, maelfu walibadilishwa” (*The Acts of the Apostles*, uk. 22).

Tunawezaje kuyeyusha mioyo? Hatuwezi. Lakini Yesu anaweza. Na tunapojazwa na Yesu (tazama Waefeso 3:14-19), upendo wake huyeyusha mioyo kupitia kwetu sisi. Kazi hii yenye nguvu ya Roho itatokea tena ndani ya kanisa. “Matukio haya yatarudiwa, na kwa nguvu kubwa zaidi. Kumwagwa kwa Roho Mtakatifu katika ile siku ya Pentekoste ilikuwa ni mvua ya vuli, lakini mvua ya masika itakuwa kubwa zaidi. Roho anasubiri uhitaji wetu na mapokezi. Kristo atadhahirishwa tena katika ukamilifu wake kwa nguvu za Roho Mtakatifu” (*Christ Object Lessons*, 121).

Tambua kwamba nguvu ya Mungu siyo nguvu nyepesi au tupu, ni upendo wa Yesu wa kina na unaojumuisha wote kwa ajili yangu na yako. Kuelewa hilo na kulipokea ndani ya moyo hubadilika na kuwa nguvu kuu ya Roho kwa ajili ya kumaliza kazi. Ilitokea miaka elfu mbili iliyopita. Itatokea tena. Mtazame Mwokozi.

*Ron E. M. Clouzet, DMin, ni katibu mstaafu wa divisheni na kwa sasa ni mchungaji katika Kanisa la Waadventista wa Sabato East Ridge.*

## **Changamoto ya Moyo**

Je, ni shauku yako kupata uzoefu wa Matendo 1 wa Jumuiya na Kalvari ili uweze kuwa tayari kwa ajili ya uzoefu wa Matendo 2 wa Mvua ya Masika? Je, unatamani moyo uliojawa na upendo wa Mungu, na maisha ambayo yanaweza kutumiwa kama daraja la upendo wa Mungu kwa wale wanaozunguka?

Habari njema ni kwamba, Yesu anafurahia zaidi kukuongoza wewe, familia yako na jamii ya kanisa lako katika uhalisia huo. Kwa nini usitumie muda kuomba sasa, ukimuomba Yesu ufunuo mpya na wa wazi wa Kalvari, ili njia iweze kuandaliwa kwa ajili ya kumwagwa kwa Roho ndani yako na kwa kanisa?

## **Mambo ya Kuombea**

- Muombe Mungu aweze kusafisha moyo dhidi ya mawazo yenyе kuvuruga na hisia zenyе kupenyeza.
- Omba ili Yesu ajidhihirishe kwako kupertia katika kujifunza msalaba.
- Omba Roho Mtakatifu aweze kukujaza kila siku, akuandae ili kuwa chombo kilicho tayari kwa ajili ya kumwagwa kwa mvua ya masika.
- Omba kwamba Mungu apate kutusaidia sisi kufahamu maana ya kuwa jumuiya katika maombi, na jinsi ya kutengeneza mnyororo wa maombi duniani.
- Omba kwa ajili ya chumba cha maombi ya mtandaoni kinachofanyika katika hizi Siku 40 za Maombi, pamoja na wakati wa mukutano wa Halmashauri Kuu:  
<https://247unitedprayer.org>

## **Vyanzo vingine vya kukusaidia kuzama kwa kina.**

- [Clearing the Way for the Holy Spirit to Work](#)
- [Promises for the Outpouring of the Holy Spirit](#)

## **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupertia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:  
<https://247unitedprayer.org>

## Siku ya Ishirini na Tisa – May 31

### Msaidizi wa Kimbingu

*"Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu."* – Yohana 16:7

*Roho Mtakatifu alikuwa ni zawadi ya juu zaidi ambayo angeweza kusihii kutoka kwa Baba Yake kwa ajili ya kuinuliwa kwa watu wake. Roho alitakiwa kutolewa kama wakala wa kuongoa, na bila hii kafara ya Kristo asingekuwa na faida... Dhambi ingeweza kuepukwa na kushindwa kupitia tu kwa uwakala wenye nguvu wa Nafsi ya Tatu ya Uungu pekee, . . . Ni Roho ndiye anayefanikisha kile kilichofanywa na Mkombozi wa dunia. Ni kupitia kwa Roho ndipo moyo hufanywa kuwa safi. Kupitia kwa Roho muumini huwa mshiriki wa asili ya kimbingu. Kristo ametoa Roho Yake kama nguvu ya kimbingu ili kushinda tabia zote za kurithi na zilizokuzwa kulekea katika uovu, na kuingiza tabia yake mwenyewe kwa kanisa lake. Yesu akizungumza kuhusu Roho alisema, 'Atanitukuzza Mimi.'* – The Desire of Ages, uk. 671.

### Changamoto ya Moyo

Je, umetumia muda wa kutafakari kwa hakika na kushukuru kwa zawadi ya pekee ya Roho Mtakatifu? Yeye ni sehemu ya Utatu Mtakatifu, Uungu, na alitumwa kwako kama zawadi kutoka kwa Yesu. Huzungumza, huongoza, hushawishi, husaidia, hufariji, hubadilisha na kutia moyo katika safari ya kuelekea mbinguni. Anakusaidia kuwa zaidi kama Mwokozi wetu mwenye upendo.

Je, umewahi kumkaribisha Roho Mtakatifu katika maisha yako? Je, umepitia uzoefu wake "akifanikisha kile kilichotolewa na Mwokozi wa ulimwengu"?

Kwa nini usianze kusihii kwa dhati kwa ajili ya ubatizo wa kila siku wa Roho Mtakatifu? Mwalike Yesu aishi ndani yako na kufanya kazi kupitia kwako, kwa Roho Mtakatifu, na mpatie ruhusa ya kufikia kila eneo la maisha yako.

### Mahitaji ya Maombi

- Omnia tua Mungu aweze kukusaidia kuelewa vema zaidi mafundisho ya kibiblia ya Uungu na ubatizo wa Roho Mtakatifu pamoja na uelewa wa kina wa aslili binafsi ya kazi ya Roho Mtakatifu.
- Omnia ili nguvu ya Roho Mtakatifu iweze kupata ushindi dhidi ya tabia za kurithi na zile zilizojengwa za kuvuta katika dhambi.

- Ombo kwamba uweze kuwa wakili mwaminifu wa muda na zaka yako. Hata kama nyakati ni ngumu Biblia inatuambia kwamba wale wanaomheshimu Mungu, yeeye atawaheshimu (1 Samweli 2:30).
- Ombo kwa ajili ya roho njema ya umoja kati ya wajumbe wa mkutano wa Halmashauri Kuu, watakaokuwa na mawazo yoyote tofauti. Ombo kwamba wajumbe waweze kukubali kwa unyenyekevu matokeo, hata kama yanaweza yasiwe kulingana na matakwa yao binafsi.
- Ombo ombi la Yesu katika Yohana 17 kwamba sisi sote tuwe wamoja. Kwa ajili ya ndoa zilizokamilishwa, familia na makanisa yenye ulinganifu, yote katika mapenzi ya Mungu.

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

## **Siku ya Thelathini – Juni 1**

### **Muunganiko Unaokoa**

*“Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu. Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini mimi; kwa habari ya haki, kwa sababu mimi naenda zangu kwa Baba, wala hamnioni tena kwa habari ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa.” – Yohana 16:8-11*

Zawadi ya Roho Mtakatifu haijatengwa kwa ajili ya umri wowote au mbari yoyote. Kristo anatangaza kwamba ushawishi wa kimbingu wa Roho Mtakatifu ulipaswa kuwa na wafuasi wake hadi mwisho. Tangu siku ya Pentekoste hadi wakati wa sasa, Mfariji ametumwa kwa wote waliojisalimisha kikamilifu kwa Bwana na huduma yake. Kwa wote waliomkubali Kristo kama Mwokozi binafsi, Roho Mtakatifu amekuja kama mshauri, mtakasaji, kiongozi, na shahidi. – Acts of the Apostles, uk. 49

### **Changamoto ya Moyo**

Sehemu ya kazi ya Roho Mtakatifu ni kuhakikisha kwa habari ya dhambi, haki, na hukumu. Vipengele hivi vitatu vya “kazi yake ya uhakikisho” vinawakilishwa na Hekalu na huduma zake.

Katika ua wa nje kafara ya dhambi ilifanyika (ikielekeza kwa Yesu msalabani na haki yake); katika Patakatifu vipengele vitatu vya kupata haki ya Kristo vilidhihirishwa – katika Meza ya Wonyesho (Kujifunza Biblia), Madhabahu ya Kufukiza Uvumba (Maombi), na Kinara cha Taa (Ushuhudiaji uliojawa na Roho). Vipengele vyote hivi vitatu vilitolewa mfano katika maisha ya Kristo kama mfano wetu leo; Na katika Patakatifu pa Patakatifu tunakumbushwa kuhusu umuhimu na uhalisia wa hukumu kwani Kuhani Mkuu aliingia katika Siku ya Upatanisho tu (ikielekeza kwa Yesu akijihuisha na hukumu ya upelelezi kwa niaba yako).

Je, unaelewa umuhimu binafsi wa kazi nzuri ya Roho Mtakatifu? Je, kwa furaha utaikubali kazi yake na kumruhusu kukuongoza kwa Yesu, na pia kukufanya kuwa kama Yesu katika tabia kadiri tunavyoishi katika wakati wa hukumu?

### **Mambo ya Kuombea**

- Omba kwa ajili ya Roho Mtakatifu kufanya kazi katika maisha ya majina 7 katika orodha yako.
- Omba kwa ajili ya Roho Mtakatifu kufanya kazi katika eneo lolote katika maisha yako linalohitaji uponyaji wa kiroho.
- Omba kwamba Roho Mtakatifu aweze kukusaidia kumpenda na Kumtii Mungu na Neno lake.
- Omba kwamba katika shauku yetu ya kutafuta namna za kibunifu za kuwashuhudia wengine, tusipoteze utegemezi wetu kwa Kristo, Neno lake, Haki yake, huduma yake ya hekalu, na nguvu yake iokoayo katika pambano kuu.
- Omba kwa ajili ya wanyonge na wenye hatari wanaokuzunguka, hasa yatima na wajane, na wale walio utumwani.

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kuititia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:  
<https://247unitedprayer.org>

## **Siku ya Thelathini na Moja – Juni 2**

### **Mfano wa Tabia ya Yesu**

*"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria." – Wagalatia 5:22-23*

*Unapopokea Roho wa Kristo – Roho ya upendo usio wa kibinafsi na kuwatumiki wengine – utakua na kuzaa matunda. Neema ya Roho itakomaa katika tabia yako. Imani yako itaogezeka, uhakikisho wako utakuwa wa kina zaidi, upendo wako utafanywa kuwa mkamilifu. Utaakisi zaidi na zaidi tabia ya Kristo katika yale yote yaliyo safi, yenye heshima, na ya kupendeza... Tunda hili haliwezi kuharibika kamwe, lakini litazaa mavuno ya uzima wa milele. – Christ's Object Lessons, uk. 67-68*

### **Changamoto ya Moyo**

Roho hutuongoza kwa Yesu. Na kadiri tunavyokaa ndani ya Yesu kupitia katika ujazo wa kila siku wa Roho Mtakatifu, atajenga ndani yetu tabia ambayo kila siku huakisi zaidi tabia ya Mwokozi wetu isiyo na ubinafsi, yenye kujisalimisha na ya upendo. Ni mchakato wa kubadilishwa kwa maisha yote. Kama ilivyo kwa embe halitokei saa moja baada ya mbegu kupandwa lakini huchukua muda kukua na kuwa mti ambao hatimaye huzaa matunda, hivyo pia kazi ya utakasaji ni mchakato unaotumia muda. Lakini amini kwamba kwa kukaa ndani ya Kristo na kwa kuwa mwaminifu kwa Neno lake kila kipengele cha tunda la Roho kitakuwa dhahiri katika maisha yako, hakuna hata kimoja kitakachokosekana!

Je, umemruhusu Roho Mtakatifu kukuza tunda lake ndani yako? Je, kuna namna umekuwa ukipinga ukuaji wa tunda la Roho ndani yako? Je, ni shauku yako kumuakisi Yesu zaidi na zaidi hadi kile watu wanachoona ni tabia yake ya upendo ndani yako?

### **Mambo ya Kuombea**

- Ombe Mungu akuze ndani yako tunda la Roho – kila kipengele chake.
- Ombe kwamba Mungu akuonyeshe ikiwa kuna maeneo mahususi katika maisha yako ambapo umepinga kazi ya Roho.
- Ombe msamaha ikiwa umemhuzunisha Roho.
- Ombe maelfu ya makundi ya kikabila duniani, yanayounda asilimia 69 ya idadi ya watu duniani, ambao bado hawana ufahamu wa wazi wa Yesu. Ombe kwa ajili ya njia mpya za kibunifu za kuwafikia.

- Ombea mikakati ya Utume katika Miji duniani. Mfano wa miradi kadhaa maalumu n Calcutta, India, Tokyo, na Japan ambapo kazi yetu hukabiliwa na changamoto nyingi kubwa. Ombea timu zinazofanya kazi kwa bidii katika maeneo haya.

**Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

## Siku ya Thelathini na Mbili – Juni 3 Ushuhuda wa Don MacLafferty

### **“Roho Mtakatifu Anapotawala”**

Na Don MacLafferty

Mwanamke mmoja alinikaribia mimi na April mke wangu kwa aibu, mwishoni mwa mikutano ya uamsho katika kanisa dogo kwenye uwanda wa Alberta, Canada. “Mnaweza kuja na kuleta uamsho katika kanisa langu?” aliuliza. “Tunahitaji uamsho haraka!”

“Mwambie mchungaji wa kanisa lako aniite, na ikiwa Mungu atatuita kuja katika kanisa lako, tutakuja.” Nilimhakikishia. Miezi ilipita. Hakuna kitu. Tuliendelea kuomba kwa ajili ya kanisa lake.

Siku moja, mchungaji alinipigia simu na kunialika kwenda na kuzungumza na viongozi wake. Niliendesha gari katika thelufji, nikiomba kadiri nilivyosafiri. Niliingia ndani ya kanisa na kutetemeka. Nilitembea katika njia yenye giza na hatimaye nikakuta chumba pembeni chenye duara dogo la viongozi waliokata tamaa, wakisubiri kuzungumza.

Baada ya ombi fupi, nilikaribishwa kushiriki. Nilieleza kile tulichoona Mungu akitenda katika makanisa na shule nyingine. Kwa furaha nilishiriki kuhusu nguvu ya Mungu ya kuita wote katika toba, msamaha, na kuishi maisha yaliyobadilishwa. Kundi lile lilisikiliza kwa ukimya. Ukimya mkubwa sana.

“Tafadhali nielezeni kuhusu kanisa lenu,” nilialika.

Mmoja alianza kwa kusema, “juma la uamsho kamwe haliwezi kufanya kazi hapa!” Sauti zingine zilidakia: “Daima tuna kazi nyingi sana kiasi cha kushindwa kuja zaidi ya siku moja au mbili.” “Tumegawanywa kabisa na utamaduni na nchi tulizotokea. Hatukutani

pamoja kwa kitu chochote." Hatimaye, kiongozi mwingine aliunganisha yote: "Uamsho hautatokea hapa."

Nilivuta pumzi, nikiomba akilini mwangu, na kuitikia, "Mungu anaweza kufanya chochote. Hakuna kisichowezekana kwa Mungu." Viongozi walitazama sakafuni, wakanishukuru kwa kufika, na kunisindikiza mlangoni.

Lakini Mungu aligusa moyo wa kiongozi mmoja au wawili pale. Walianza kuomba. Waliomba na kuomba. Mungu alisikia. Nilipokea mwaliko wa kwenda na kuhamasisha uamsho, na Mungu aliniita mimi na April tuweze kwenda!

Tuliomba kwamba wakusanyike kwa maombi wengi kadiri itakavyowezekana kabla ya uamsho ili kuomba na kufundishwa kuwa viongozi wa vikundi vidogo. Walikubali. Tulienda siku tuliyokubaliana na kutembea kuingia katika kanisa lile kubwa, tukitegemea kukuta wabia wa maombi takribani thelathini au arobaini. Mtu mmoja alikuwa akifanya kazi kwa bidii ili kuandaa eneo la mkutano. Hatimaye, watu nane au tisa walifika. Wengi wao walichelewa. Walisema kwa hakika haukuwa usiku sahihi wa kuja. Tuliomba nao, na kuwawezesha, kisha tukaondoka kanisani tukiwa tumeguswa kweli.

Mungu alitugusa kuja na kuomba na kuwafundisha watu kwa mara ya pili. Kanisa lilahidi kutafuta watu wengi zaidi. Katika siku iliyopangwa kwa ajili ya mafunzo, tulifika tukiwa na tumaini na matarajio zaidi. Lakini, walifika wachache zaidi ya siku ya kwanza. Lakini tulipiga magoti na kuomba na kudai ahadi za Mungu.

Kijana mmoja mdogo, nitamuita Dex, alikuwa ameketi Jirani na mama yake katika mduara wa maombi. Alipunga mkono ili kupata umakini wangu. "Je, ninaweza kuwa kiongozi wa kikundi kidogo?" aliropoka. Alikuwa mdogo, mdogo sana, lakini bado alikuwa na shauku zaidi ya uamsho kuliko hata watu wazima wakichanganywa wote pamoja.

"Ndiyo, unaweza!" nilimhakikishia. "Ungana na mama yako. Mnaweza kufanya kazi pamoja." Tabasamu lake lilikuwa kubwa kuliko mwezi. Macho ya mama yake yaling'aa kwa machozi. Mungu alinong'ona moyoni mwangu, "Mtoto mdogo atawaongoza."

Usiku wa kwanza wa uamsho ulifika. Dex na mama yake walikaa mbele wakiwa na mduara wa viti, nilipoita kwa ajili ya uamsho. Waliongoza kikundi chao kidogo katika Neno na maombi. Roho Mtakatifu alikuwepo.

"Kesho usiku watakuja watu wachache zaidi" mhudhuriaji mmoja alitabiri, kadiri alivyokuwa akiondoka katika mkutano ule wa kwanza. Lakini tulienyelea mbele. Kila siku, wachache wetu tuliomba kwa ajili ya kila mshiriki katika kanisa lile, iwe bado anakuja kanisani au la. Tulimuomba Mungu aguse moyo wa kila mtu kwa upendo na

nguvu ya Roho Mtakatifu. Tulimuomba Mungu afanye kila ambacho yeye peke yake ndiye awezaye kufanya.

Na kila usiku, watu walikuja, si wawili au watatu, lakini wengi. Walikuja wadogo na wakubwa. Watu walikuja kutoka kazini wakiwa na nguo zao za kazi. Watu walikuja ambao hawakuwa wamehudhuria kanisa kwa muda mrefu. Kadiri Roho Mtakatifu alivyogusa miyo, watu walianza kutembea katika chumba kile. Waliwafikia watu ambao hawakuwahi kuzungumza nao au kuketi pamoja kwa ajili ya chakula kabla ya mikutano hii. Watu waliokuwa wamegombana waliungama na kuomba msahama. Watu wenye miyo migumu waliruhusu miyo yao kufunguliwa ili kupokea upendo wa Mungu, wengine kwa mara ya kwanza.

Roho Mtakatifu alikuwa akifanya kazi! Mungu alikuwa akiangaza gizani, apate kuwakusanya wale waliokuwa wametawanyika ili kuwa familia ya Mungu kwa mara nyingine. Hilo ndilo analolifanya Roho Mtakatifu!

*Don MacLafferty ni mwasisi/mwenyekiti wa ‘In Discipleship’ (Katika Uanafunzi). Mungu amegusa moyo wa Don na April mke wake ili kuwaita vijana na watu wazima katika uamsho wa kila siku pamoja na Yesu kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu. Wanahamasisha makanisa na shule kuungana katika kuwawezesha wazazi kuwafanya watoto wao kuwa wanafunzi na kuwaandaa kwa ajili ya utume.*

### **Changamoto ya Moyo**

Maombi na uamsho vinaenda sambamba. Ushuhuda wa leo umeliweka hilo wazi kabisa. Mambo kanisani kwako yapo vipi? Kuna ukosefu wa uamsho? Je, inawezekana ni kwa sababu kuna uhaba wa maombi ya dhati? Je, Mungu anakuita kuanza kuomba kwa ajili ya uamsho katika kusanyiko lako? Kwa nini usitafute m-bia wa maombi katika kanisa lako, na muombe Mungu awaongoze kadiri mnavyoombea watu, hali, na uamsho kwa ujumla wa kanisa lako mahalia?

Hebu fikiria tu kile ambacho kitatokea tunapomruhusu Roho Mtaktifu kufanya kazi katikati yetu!

### **Mambo ya Kuombea**

- Ombo kwa ajili ya uamsho katika kanisa lako na kwamba m(wa)chungaji na m(wa)zee waweze kujazwa na Roho.
- Ombo kwamba Mungu aweze kukupatia rafiki wa maombi, au hata marafiki wawli wa maombi ili kuombea uamsho.
- Ombo ili Roho Mtakatifu aweze kumwagwa kwa viongozi wa divisheni yote, unioni, konferensi, na kanisa mahalia, pamoja na katika huduma zinazotegemeza au uongozi.

- Omba kwamba uweze kuitikia kwa namna yoyote ile Roho Mtakatifu atakavyoongoza, hata ikimaanisha kutoka na kwenda kwa Imani, pengine hata kuvuka "Mto wa Yordani."
- Dai ahadi za Ezekieli 36:25-27 na Ezekieli 37 na mtazame Mungu akileta uamasho wa kweli. Watu waliokufa kiroho na makanisa yanaweza kuishi kwa Roho Mtakatifu!
- Omba kwa ajili ya majina 7 katika orodha yako ya maombi.

## Siku ya Thelathini na Tatu – Juni 4

### Sabato ya Mambo ya Kuombea

- Omba kwamba kiwango kikubwa zaidi cha Roho Mtakatifu kiweze kumwagwa katika maisha yako Sabato ya leo.
- Ombea wale walio peke yao, au wanaopambana katika mazingira ya kujifungia, kama miji ya Kichina. Omba kwamba waumini wote wawewe kuhisi ukaribu wa Yesu bila kujali hali zao.
- Ombea makundi ya watu ambao hawajafikiwa ambalo Mungu ameweka ndani ya moyo wako. Omba kwa ajili ya mbinu unazoweza kutumia kulisimamia kundi hilo au njia unazoweza kutumia kuwafikia kwa namna halisi.
- Omba kwamba wito wa "Yesu Anakuja! Jihusishe!" uweze kuwa na kipaumbele kikubwa katika maisha ya kila siku ya kila mmoja wetu.
- Ombea huduma za vyombo vyetu vya habari duniani, Hope Channel, 3ABN, na vingine vingi, kwamba viendelee kusambaza ukweli wa Mungu mbali zaidi na kwa upana zaidi.

## Siku ya Thelathini na Nne – Juni 5

### Jumapili ya Mambo ya Kuombea

- Omba kwa ajili ya Mkutano wa Halmashauri Kuu huko St. Louis, Marekani unaoanza leo.  
Ombea usalama katika safari pamoja na maandalizi ya moyo kwa wajumbe
- Omba kwa ajili ya mbaraka wa pekee wa Roho Mtakatifu katika vikao na maamuzi yatakayofanyika.
- Omba kwa ajili ya timu ya uandaaji wa mkutano ili mipango yote iweze kufanikiwa vizuri kwa ajili ya wajumbe watakaohuduria kwa njia ya mtandao.

- Omba kwa ajili ya chumba cha maombi kwenye eneo la mukutano, ambacho wengi watatumia kwa ajili ya maombi.
- Omba kwa ajili ya viongozi wa Konferensi Kuu ili wawe na hekima ya Roho Mtakatifu katika jinsi ya kuendeleza utume wa kanisa la Mungu na viongozi gani wanaopaswa kuchaguliwa kwa ajili ya siku za usoni.

**Vyanzo vingine vya kukusaidia kuzama kwa kina.**

[Learning to Walk by Faith: Conversations with Don MacLafferty](#)

**Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:  
<https://247unitedprayer.org>

**Juma la 6: Juni 6 – 11**

**Siku ya Thelathini na Tano – Juni 6 – Wazo la Kesha: Ujumbe wa Malaika Watatu**

### **“Ombi la Wakati wa Mwisho”**

Na Mark Finley

Japokuwa maombi yamekuwa katika moyo wa kanisa la Kikristo kwa karne nyingi, ni muhimu zaidi katika saa hii ya hatari ya historia ya dunia. Shetani ameachia roho za kishetani ili kuleta madanganyo, matatizo, na vifo katika sayari yetu. Mungu hatashtukizwa. Atamwaga Roho yake kwa nguvu ya mvua ya masika kwa kanisa lake linaloomba. “Kilio kikuu” cha malaika wa tatu wa Ufunuo kitasikika toka upande mmoja wa dunia hata upande mwagine.

Mtume Yohana anasema, “Baada ya hayo nalionna malaika mwagine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake” (Ufunuo 18:1).

Malaika watashuka kutoka katika uwepo wa Mungu wenyе utukufu katika kiti cha enzi wakiwa na amri ya kuonya wakazi wa dunia kwa kile kinachoujia ulimwengu. Mafungu yanasema kwamba malaika huja na “mamlaka kuu.” Neno la Kigiriki katika Agano Jipyaa la mamlaka ni “Exousia.” Yesu hutumia neno hili katika injili ya Mathayo katika uwiano na kuwatuma wanafunzi wake. Katika Mathayo 10:1 Yesu anawapatia wanafunzi wake “mamlaka” dhidi ya kanuni na nguvu zoe za kuzimu. Anawatuma nje wakiwa na nguvu

ya kimbingu ili wawe washindi katika vita kati ya wema na uovu. Katika Mathayo 28 fungu la 18, kwa mara nyingine anawatuma lakini wakati huu anawatuma na "mamlaka yote mbinguni na duniani kwenda na kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi" (Mathayo 28:18).

Wanafunzi walipotoka katika kipindi chao cha maombi katika chumba cha juu siku ya Pentekoste, walikwenda kwa mamlaka ya Kristo aliye hai. Kwa miaka michache, wanafunzi waliitangaza injili kwa dunia inayofahamika sasa. (Wakolosai 1:23)

Katika wakati wa mwisho Roho Mtakatifu atamwagwa kwa watu wanaoomba kwa nguvu ambayo haijawahi kutokea. Injili itasambaa kwa haraka sana katika miisho ya dunia. Maelfu watabadilishwa kwa siku moja. Neema na ukweli wa Mungu utaiathiri sayari yote.

Ibilisi hatajisalimisha bila pambano kubwa. Muda si mrefu tutaingia katika pambano la vizazi kati ya wema na ubaya. Ushauri wa Paulo kwa Waefeso huzungumza nasi kwa msisitizo unaofaa leo. "Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake... Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho." (Waefeso 6:10-12)

Tupo katika vita halisi kati ya wema na uovu. Ushauri wa Paulo ni upi, "Mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake."

Katika vita hii Yesu ndiye nguvu yetu katika udhaifu. Yesu ndiye nuru yetu gizani. Yesu ndiye ushindi wetu katika majoribu. Yesu ndiye tumaini letu katika kukata tamaa. Yesu ndiye jemedari wetu mkuu. Mtu Paulo anatukumbusha kwamba "...silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome" (2 Wakorintho 10:4).

Katika Kristo, ibilisi ni adui aliyeshindwa. Chochote kitakachoshambulia uso wako, jaribu lolote ambalo mwovu atarusha kwako, changamoto yoyote unayokabiliana nayo, magumu yoyote unayopitia, unaweza kumkabili Shetani kwa Jina la Yesu. Kamwe hajawahi kushindwa vita kati yake na ibilisi. Ndiye mshindi mkuu anayeangusha ngome za kuzimu, akikanyaga nguvu za uovu na kumshinda adui kwa niaba yetu. Kupitia maombi kuna nguvu katika Yesu ya kumshinda ibilisi kila wakati.

*Mark Finley, mwinjilisti wa kidunia, mwandishi na msaidizi wa Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu.*

### **Changamoto ya Moyo**

Ikiwa kumewahi kuwapo wakati ambapo watu wa Mungu wanahitaji kujihusisha katika maombi mengi, ni sasa. Tunaishi katika siku za mwisho na tunakabiliwa na matukio ya mwisho. Shetani anatamani sana kuliharibu kanisa na washiriki wake. Hofu yake kubwa

ni kwamba waumini wataunganishwa na Yesu kwa kina na kumtukuza yeye kupitia maisha ya upendo, ukweli, na huduma.

Kwa mashambulizi yoyote kutoka kwa Shetani unayoweza kukabiliana nayo, unaweza kumwamini Yesu aweze kukutetea.

Je, unatamani ile Imani ya wakati wa mwisho yenyе ushindi itakayosimama licha ya jaribu lolote? Kwa nini usitumie muda wa ziada katika maombi na Yesu siku ya leo, ukinywa kutoka katika Chemchemi ya Uzima, upendo na ukweli, na kuwezeshwa kwa ajili ya huduma kwake katika siku hizi za mwisho?

### **Mambo ya Kuombea**

- Omba Mungu ajenge ndani yako Imani ya wakati wa mwisho inayotenda kazi kupitia upendo.
- Omba kwa ajili ya uvumilivu wa kiroho, kupitia muunganiko wenye nguvu na Yesu, il kupinga na kustahimili mashambulio na majaribu ya ibilisi.
- Omba ili Roho Mtakatifu awezae kubariki vikao vya siku ya leo vya Mkutano wa Konferensi Kuu pamoja na maamuzi mengi ya kanisa la kiulimwengu.
- Omba ili Roho Mtakatifu aweze kuongoza uchaguzi wa viongozi ambao kwa unyenyekevu wataheshimu Neno Lake na kuendeleza utume wa kanisa bila ubinafsi.
- Omba kwamba watu wengi waweze kutembelea vyumba vya maombi vya mkutano wa Konferensi Kuu katika eneo la mkutano na mtandaoni.

**Vyanzo vingine vya kukusaidia kuzama kwa kina.**

[The Difference between True and False Revival – by Mark Finley](#)

**Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa:  
<https://247unitedprayer.org>

### **Siku ya Thelathini na Sita – Juni 7**

#### **Malaika wa Kwanza**

*“Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakao juu ya nchi, na kila taifa na kabilia na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji.” – Ufunuo 14:6-7*

*Wajibu wa kumwabudu Mungu umejengeka katika ukweli kwamba yeye ni Muumbaji na kwamba watu wote wanategemea uhai kutoka kwake. Na popote, katika Biblia, yanapowasilishwa madai yake ya utii na ibada, juu ya miungu ya wapagani, umeonyeshwa ushahidi wa nguvu yake ya uumbaji.* – Lift Him Up, uk. 51

### **Changamoto ya Moyo**

Waadventista wa Sabato wana wito wa pekee, wa kinabii wa kutangaza kwa maneno na matendo Ujumbe wa Malaika Watatu kwa dunia yote katika maandalizi ya Ujio wa Yesu kwa Mara ya Pili. Msingi wa Ujumbe wa Malaika Watatu ni injili ya milele. Habari njema kwamba Yesu *ni* Mwokozi wako. Kwa kumpokea kwa Imani iliyo hai, unapokea utakaso wa, na ushindi dhidi ya dhambi, na uzima wa milele.

Ujumbe wa malaika wa kwanza unaweza kufupishwa hivi: Mungu ni Muumbaji wako. Ndiyo maana unapendwa na kutamaniwa naye na hauhitaji kujiabudu au kuabudu aina yoyote ya miungu. Kama uumbai wake na kwa kuitikia upendo wake, unawezeshwa kuakisi tabia yake ya upendo, hasa sasa kadiri tunavyoishi katika siku za hukumu.

Je, utashikilia utambulisho wako wa wakati wa mwisho katika Yesu na kumruhusu kuishi maisha yake ndani yako? Je, unaamini kwamba uhusiano huu wa karibu na Yesu unaweza kukupatia ujasiri katika hukumu?

### **Mambo ya Kuombea**

- Ombea ili Mungu atukuzwe katika maisha yako kama Muumbaji na Mkombozi.
- Ombea kwa ajili ya uelewa wa wazi zaidi wa utambulisho wako wa wakati wa mwisho ndani ya Yesu.
- Ombea kwamba Mungu akusaidie kufahamu ni kwa nani unapoweza kuweka Imani yako kwa usalama katika kipindi hiki cha hukumu.
- Ombea kaka na dada zetu wanaoishi katika maeneo yenye migogoro ya kiserikali na ugandamizwaji wa kidini.
- Ombea kuhusu jinsi unavyoweza kuwategemeza waumini katika sehemu hii ya dunia.

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

## Siku ya Thelathini na Saba – Juni 8

### Malaika wa Pili

*“Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mwinyo ya ghadhabu ya uasherati wake.”* – Ufunuo 14:8

*Mungu bado ana watu katika Babeli; na kabla ya kuja kwa hukumu yake ni lazima hawa waaminifu waitwe kutoka, ili wasishiriki dhambi zake na “kupokea mapigo yake.”* – Maranatha, uk. 171

### Changamoto ya Moyo

Ujumbe wa malaika wa pili ni mfupi lakini ulio wazi: Dunia hii na mifumo yake yote ya Imani, taasisi, harakati, zilizovunjika na za uongo, zimeharibiwa, haziwezi kutegemewa na zimeanguka.

Mwitikio pekee kwa ukweli huu unaokata ni kuificha Imani yako katika Mwamba Imara, Muumbaji wetu na Mkombozi wa wanadamu wote – Yesu. Na wakati Babeli ikiwa imeanguka kweli, bado kuna watu katika Babeli ambao wamegundua uhalisia huu na ni watafutaji wa kweli, nao wanaosubiri wito wa kweli, ili waweze kutoka.

Unaweza kuwa umeshatoka katika Babeli tayari, lakini je, Babeli imetoka ndani yako? Au bado kuna maeneo katika maisha yako ambapo unaweka Imani yako katika mifumo iliyovunjika ya dunia hii? Kwa nini usisalimishe yote leo? Kwa nini usichukue hatua moja zaidi na kuungana na Yesu katika kuwaita watu kutoka katika meli hii inayozama?

### Mambo ya Kuombea

- Ombo kwa ajili ya uelewa wa kina zaidi wa Ujumbe wa Malaika Watatu.
- Ombo ili Mungu atoe kitu chochote cha “Kibabeli” kilichoko katika moyo wako, na kukupatia ujasiri wa kuwaita watu watoke katika mkanganyiko wa kiroho.
- Ombo kwa ajili ya kikao cha leo cha Mkutano wa Konferensi Kuu pamoja na maamuzi yake kwa kanisa la kiulimwengu.
- Ombo kwa ajili ya Huduma za Vijana za Konferensi Kuu, na huduma za vijana katika kanisa lako mahalia ili ziweze kutumika kuwarejesha watoto wetu kwa Yesu.
- Ombo kwa ajili ya baadhi ya maeneo ya dunia yaliyo magumu na ambayo hayajafikiwa. Ombo ili Roho wa Mungu aweze kuvunja ngome hizo kwa nguvu na miujiza yake mikuu.
- Ombo kwa dhati kwa ajili ya majina yako 7. Usikate tamaa!

## **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

## **Siku ya Thelathini na Nane – Juni 9**

### **Malaika wa Tatu**

*"Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo. Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake. Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." – Ufunuo 14:9-12*

*"Mungu anakualika kwa mkono mmoja, Imani ishikilie mkono wake wenye nguvu, na kwa mkono mwingine upendo, fikia roho zinazopotea. Kristo ndiye njia, kweli, na uzima. Mfuate yeye. Usifuate mwili, bali ifuate Roho. Tembea kama alivyotembea. Hii ndiyo nia ya Mungu, hata utakaso wako. Kazi unayopaswa kutendeka ni kufanya mapenzi yake anayetegemeza maisha yako kwa utukufu wake. Ikiwa mtajishughulisha wenyewe, haitakufaidia chochote. Kujishughulisha kwa ajili ya faida ya wengiine, kutokujijali na kwa dhati kusalimisha yote kwa Mungu, kutakubalika kwake na kurejeshwa kwa neema yake kuu." – Testimonies, Gombo la 2, uk. 170*

### **Changamoto ya Moyo**

Shetani, mwanzilishi wa kifo, mateso, ubinafsi, maumivu, dhambi, na wote wanaokumbatia madanganyo yake vitaharibiwa katika hukumu ya mwisho, ili haki na upendo viweze kurejeshwa katika ulimwengu. Wale tu watakaomtumainia Mwokozi mwenye upendo Yesu Kristo ndio wataokolewa milele na kubadilishwa kuwa watu wapya wanaoakisi upendo wa Mungu usio na ubinafsi. Baada ya muda hakutakuwa na fursa zaidi ya kuivuta roho iliyopotea kwa ajili ya Yesu.

Je, ni shauku yako leo, kufanya yale yote yaliyo katika uwezo wako ili kuifikia dunia hii iliyopotea kwa upendo wa Mungu, na ujumbe wa ungamo, wokovu, na hukumu? Je, utang'aa kama mwakilishi wa Kristo katika dunia yenye giza? Je, utasimama, utaishi,

utazungumza, utajali, utabariki, utapenda, na kufurahia utambulisho wako wa kinabii kama muumini wa kanisa la Waadventista wa Sabato? Na ikiwa bado wewe siyo muumini wa kanisa hilo, je, ni shauku yako kujunga na harakati za Mungu za wakati wa mwisho, kufuata Neno la lake, kubatizwa, na kujihusisha katika utume maalumu wa Yesu kwa ajili yako?

### Mambo ya Kuombea

- Ombo kwa ajili ya uelewa wa Ujumbe wa Malaika wa tatu.
- Ombo kwa ajili ya nguvu ya kutii Neno la Mungu vyovyyote vile atakavyokuongoza.
- Ombo kwa ajili ya moyo wa utume na huduma.
- Ombo kwamba Yesu aongeze Imani yako kwake na yeye ang'ae kupitia kwako.
- Ombo kwa dhati kwa ajili ya majina 7, pia kwa ajili ya majirani zako ambao hawajaokolewa wanaoishi karibu nawe.

### Junge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.

Junge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

## Siku ya Thelathini na Tisa - Juni 10 Ushuhuda wa Dan Serns

### “Injili ya Milele Ilibadilisha Maisha ya Bill”

Na Dan Serns

Muda mfupi baada ya kuhamia katika mtaa mpya, mimi na mke wangu tuligundua kwamba kulikuwa na kelele sana usiku. Tulilalamika kuhusu majirahi zetu kwa muda kabla ya kuamua kuwa tunapaswa kuwaombea. Hata hatukuwa tunafahamu majina yao, lakini hata hivyo tulitengeneza orodha ya maombi.

Tuliomba kwa ajili ya “majirani wenyе boti kubwa,” waliokuwa wameegesha boti yao barabarani. Tuliomba kwa ajili ya “majirani wenyе kutukana,” waliotukana zaidi ya wengine. Tuliomba kwa ajili ya “mwanamume aliye na mbwa wawili,” ambaye daima alipita nyumbani kwetu kila jioni, akiwapigia kelele mbwa wake, ambao walikuwa wakimvuta haraka zaidi ya namna alivyotaka kutembea.

Unapomuomba Yesu mfululizo kwa ajili ya watu kwa majuma kadhaa, yeye anaweka shauku ndani ya moyo wako ya kufanya kitu kingine cha kuwasaidia. Tulizungumza na kuamua kuanzisha kikundi cha kujifunza Biblia nyumbani kwetu kila Jumanne jioni. Sisi

wenyewe tuliwaalika watu waliokuwa katika orodha yetu ya maombi. Pia tulitoa mwaliko wetu kwa nyumba nyingine zote katika mtaa ule. Na tulialika watu kutoka katika familia ya kanisa letu kuweza kujumuika nasi.

Usiku wetu wa kwanza, tulikuwa na wageni sita nyumbani kwetu: watano kutoka kanisani na "mwanamume mwenye mbwa wawili." Tilitambua kwamba alikuwa anaitw Bill na alikuwa na umri wa miaka sitini na tano akikaribia kustaafu. Bill hakusema mengi wakati wa saa moja ya kwanza tukiwa pamoja, na ilipofika muda wake wa kusoma Biblia, alisema "Pita." Lakini mwisho alitushukuru na juma lililofuata alirudi. Alirudi juma lililofuata pia, na hilo juma la tatu hakuna aliyejua isipokuwa Bill peke yake.

Kwa kuwa hakuna mtu mwingine aliyejua akihudhuria, alianza kutuuliza maswali. Swali lake la kwanza lilikuwa, "Katika miongozo yetu ya kujifunza Biblia mara nyingi kuna namba mbili zenyet doti mbili katikati yake. Hiyo humaanisha nini?" ilikuwa fursa nzuri ya kumsaidia Bill kujifunza jinsi ya kusoma na kutumia Biblia. Alishukuru sana.

Juma la nne, kila mtu alirudi, akiwemo Bill. Somo lilihusu injili ya milele kutoka Ufunuo 14. Tulijifunza jinsi ambavyo sote ni wadhabhi na tunastahili kifo, lakini Yesu alikuja kuishi na kufa na kugharimikia dhambi zetu. Tulishiriki jinsi Yesu anavyotupatia ushindi dhidi ya mapambano yetu na jinsi anavyoandaa maisha mazuri ya siku za usoni kwa ajili ya kila mmoja wetu.

Mwisho wa kujifunza, nilimwalika kila mmoja (kama alikuwa tayari) kusema, "Yesu, ninataka utawale kila sehemu ya maisha yangu." Usiku ule Bill alimwalika Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wake. Nilifurahi sana! Niliweza tu kuwaza Yesu mbinguni akimwambia malaika Gabrieli, "Anza kujenga nyumba mpya! Kuna mtu amenikubali, na ninampatia hisia ya amani ambayo hajawai kuipitia hapo kabla. Nitambadilisha, na siku moja nitamleta nyumbani katika nyumba yangu ambapo ataishi milele pamoja nami."

Majuma machache kadhaa tuligundua kwamba Bill alifariki kwa mshtuko wa moyo alipokuwa amepumzika na mjukuu wake. Mke wa Bill alituomba kuendesha mazishi. Tulipokuwa tukijiandaa na huduma hii ya mazishi iliyokuwa ya kuhuzunisha na ambayo haikutarajiwa, Sharon – mke wake, alitueleza kuwa, "Bill alipenda kujifunza Biblia nyumbani kwenu kila juma. Hakuwahi kumiliki Biblia kabla ya kuanza kujifunza nae. Lakini ilibadilisha maisha yake."

Kisa cha maisha ya Bill kimeisha, lakini ninaamini kwamba atakuwa kati ya watakaopaa kwanza katika mawingu ili kukutana na Yesu pale atakaporudi. Na tunatazamia kwa tumaini hilo.

Yesu yule yule aliyebadilisha maisha ya Bill anaweza kumbadilisha mtu yejote! Habari yetu njema, ambayo pia hujulikana kama “injili ya milele” (Ufunuo 14:6), itatangazwa kwa dunia nzima kabla Yesu hajarudi (Mathayo 24:14). Hebu tuwe jasiri katika kushiriki habari hizi njema wakati bado tuna nafasi. Hebu tusiendelee kujificha ndani au kushiriki injili hafifu ambayo hushindwa kuwaongoza watu chini ya msalaba. Injili hii nzuri ya Ujumbe wa Malaika watatu ina nguvu ya kubadilisha maisha yetu yote. Hebu tuishiriki! Yesu anakuja karibuni!

*Dan Serss ni mwenyekiti wa Konferensi ya California ya Kati.*

### **Changamoto ya Moyo**

Je, haipendezi kuona kile kinachowezekana tunapoanza kuombea wengine na kisha kuwahudumia kadiri Mungu anavyoongoza? Huwezi juu, unaweza kuwa nafasi ya mwisho ya mtu kusikia kuhusu Yesu. Kwa nini usimuombe Mungu sasa akuonyeshe watu ambaa unaweza kuwaombea na kuwahudumia katika mtaa wako. Omba uwezo wa kushiriki kweli za Ujumbe wa Malaika Watatu kwa ufanisi wa Roho Mtakatifu. Ikiwa utaomba maombi haya kwa dhati, miadi ya ajabu ya kimbingu itatokea!

Kama ulivyoomba kwa ajili ya majina 7 katika orodha yako, tunataka kukuhamasisha kuendelea kuwaombea na kuwafikia. Wahudumie. Tafuta namna ya kuwatumikia na kuwapenda kama Yesu anavyotupenda. Mungu anaweza na yupo tayari kuingia katika maisha ya watu hawa, na kadiri unavyoendelea kuomba, huleta tofauti katika dunia isiyonekana. Siku moja, kama siyo sasa, utapata majibu kwa maombi yako.

### **Mambo ya Kuombea**

- Omba ili Roho Mtakatifu aongoze katika siku za mwisho za mkutano wa Konferensi Kuu.
- Omba kwa ajili ya wale watakaoingia madarakani katika uongozi mpya, kwamba Roho Mtakatifu awawezeshe kwa ajili ya kazi iliyo mbele yao.
- Omba kwa ajili ya fursa za kuifikia familia yako, marafiki, majirani, na wafanyakazi ukiwa na injili ya Yesu.
- Endelea kuomba kwa ajili ya majina yako 7, ukitafuta namna ya kuwahudumia.
- Omba ili Mungu akupatia angalau mtu mmoja ambaye unaweza kumwelekeza kwa Kristo katika mwaka unaokuja.

## **Siku ya Arobaini – Juni 11**

### **Sabato ya Mambo ya Kuombea**

- Msifu Mungu kwa yale aliyotenda katika maisha yako kwa hizi siku 40 za maombi. Kuwa mahususi.
- Msifu Mungu kwa kile atakachotenda kupitia kwa viongozi wapya watakaochaguliwa, na watakaorudia kuchaguliwa wa kanisa la kiulimwengu kadiri wanavyokabiliana na miaka ijayo ya uongozi na mzigzo wa majukumu yake.
- Msifu Mungu kwa jinsi anavyotenda kazi, na atakavyotenda kazi, katika maiasha ya majina yale 7 uliyokuwa ukiombea katika hizi Siku 40 za Maombi.
- Msifu Mungu kwamba atakwenda kukupatia Imani ya kusimama katika nyakati za mwihi na kwamba hivi karibuni, atakuja katika mawingu ili kutuchukua nyumbani.
- Msifu Mungu kwamba ana mambo makubwa ghalani kwa ajili yako, na huu ni mwanzo tu wa safari hii ya pekee ya maisha yako!

### **Vyanzo vingine vya kukusaidia kuzama kwa kina.**

Tembelea <https://www.revivalandreformation.org> kwa ajili ya vitendea kazi vipya vinavyoendelea.

### **Jiunge katika maombi ya mtandao ya 24/7 United Prayer.**

Jiunge na waumini wengine kutoka kote ulimwenguni wanaoomba pamoja kupitia katika mtandao wa Zoom kwa siku hizi 40 za maombi kwenye tovuti hii hapa: <https://247unitedprayer.org>

Wapendwa marafiki,

Siku 40 za Maombi zinaweza kuwa zinaishia leo, lakini safari yako na Yesu itaendelea tu kuwa bora zaidi kadiri unavyomtafuta. Kama ulivyokuwa sehemu ya hii safari ya Siku 40 za Maombi, ni ombi letu kwamba umeshuhudia kwa uhakika nguvu ya Mungu katika maisha yako. Kwamba umepitia uzoefu wa Roho Mtakatifu kukuleta katika uamsho wa kweli na uzoefu unaoendelea wa matengenezo kuliko ulivuwahi kupitia hapo kabla. Na hili halipaswi kuishia mwisho wa Siku 40 za Maombi lakini linapaswa kuendelea hadi Yesu atakaporudi.

Tunakuhamasisha kuendelea kujunga na waumini wengi kutoka duniani kote katika kuomba pamoja masaa 24 kwa siku katika Zoom: <https://247unitedprayer.org>. Saa za maombi zitaendelea kwa wale wote wanaotaka kushiriki. Na usiache kuombea yale majina 7 (na mengine mengi ambayo Mungu anaweza kuleta katika moyo wako) hadi utakapoona majibu yamepatikana.

Kumbuka, "Kuwahuisha Washiriki Wote" humaanisha kila mmoja anapaswa kufanya kitu kwa ajili ya Bwana! Hebu tuisahau wazo kuu la Mkutano wetu wa Halmashauri Kuu 2022: "Yesu Anakuja! Jihusishe!"

Tuna shauku ya kusikia kuhusu shuhuda zenu za kile Mungu alichotenda katika hizi Siku 40 za Maombi katika maisha yako, familia, na kanisa lako!

Mungu akubariki!

*Timu ya Uamsho na Matengenezo*